ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu

49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde

79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili – Tarehe 4 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hati ya Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria ya Shirika la Bandari na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Salma Mussa Bilal (Kny. Mhe. Makame Mshimba, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasilisno na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari na mambo mengine yanayohusiana nayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 15

Vikosi vya SMZ Kunyanyasa Raia

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Kwa kuwa Jeshi la Polisi ndilo lenye mamlaka ya Kikatiba kulinda Usalama wa Raia na mali zao, na kwakuwa Jeshi la Polisi linatoa nafasi kwa vikosi vya SMZ kunyanyasa Raia pamoja na kuhatarisha amani ya nchi.

Je, endapo umma wa Wazanzibari nao utaamua sasa mateso basi (*enough is enough*) na kuamua kupambana na vikosi hivyo katika hali ya kujihami, jambo ambalo linaweza kupelekea uvunjifu mkubwa wa amani, kama hili likitokea nani wa kulaumiwa baina ya *IGP* na SMZ.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa unyenyekevu wa hali ya juu na kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wangu swali lake Nam. 15 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Jeshi la Polisi ndilo lenye mamlaka Kikatiba na Kisheria kulinda usalama wa raia na mali zao na kwamba wakati mwengine hushirikiana na Vikosi vya SMZ ili kufanikisha kazi hiyo.

Mhe. Spika, sio kweli kwamba Jeshi la Polisi linatoa nafasi kwa Vikosi vya
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar kunyanyasa raia na kuhatarisha amani ya nchi, bali Jeshi la Polisi hulalzimika kushirikisha vikosi maalum vya SMZ au wananchi kupitia Polisi Jamii pale tu inapokuwepo haja hiyo kutokana na ukubwa wa matukio ya vurugu ili kudhibiti hali ya amani na usalama katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hali ya amani na usalama wa nchi inahitajika sana kwa wananchi kutii taratibu za sheria nakuepuka kabisa kushabikia au kujiingiza katika vitendo vya uvunjifu wa sheria na amani katika nchi ili tuishi kwa amani na upendo.

Katika kusimamia sheria malalamiko mbali mbali hujitokeza na njia pekee ya kuyashughulikia malalamiko hayo ni kwa mujibu wa sheria sio kuchukua hatua mikononi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa sababu uzoefu unaonesha hususan katika nchi zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania, kwamba Vikosi vya Mgambo pamoja na Vikosi vya Waasi huchangia sana katika kuvuruga amani na utulivu wa nchi na hatimaye kusababisha madhara makubwa kwa raia, na kwa kuwa Jeshi la Polisi ndilo lenye dhamana ya kulinda raia na mali zao na kwa kuwa uzoefu unaonesha kwamba hapa Zanzibar baada ya matokeo mbali mbali au shughuli mbali mbali kufanyika kama vile chaguzi au walipokamatwa maamiri wa Uamsho, vikosi vya SMZ vilikuwa mbele kudhibiti fujo pamoja na kukamata raia na kuwatesa kiholela. Ushahidi unaonesha hata katika kipindi kile cha uchaguzi mdogo Bububu kuna wananchi walikamatwa na kuingizwa katika Kambi ya KMKM.

Sasa Mhe. Spika, kama wananchi watasema *enough is enough* kama nilivyoeleza kwenye swali langu la msingi. Je, wakubeba jukumu hili ni SMZ au ni IGP na Jeshi la Polisi. Hilo ni moja.

Pili Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba mambo haya yashughulikiwe Mahkamani. Je, mbona KMKM wanapokamata wananchi wanawaweka pale Kibweni bila ya kuwapeleka Mahkamani, huo ndio utawala bora.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya Katiba na Sheria na kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba pale popote panapojitokeza malalamiko au mtu kuhisi ameonewa kinyume na taratibu za sheria, basi mwananchi huyo ana haki ya kupeleka malalamiko yake katika vyombo vya sheria ili kudai haki yake. Mpaka sasa Mhe. Spika, hakuna mwananchi tuliyepata taarifa kwamba amekwenda Mahkamani ama kuripoti kwenye vituo vya polisi kuonesha kwamba ameonewa.

Napenda nitoe wito kwa mtu yeyote ambaye ameona haki yake amenyimwa au ameonewa, au amefanyiwa kitendo kinyume na utaratibu basi afuate mkondo wa sheria. Hakuna utaratibu wowote Mhe. Spika, katika nchi yenye kuendeshwa kwa mujibu wa sheria kuchukua hatua mikononi mwake ni kosa la kisheria unapoamua kufanya hivyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa siku za hivi karibuni kulitokea vurugu ambazo zilisababisha mali za serikali kuharibiwa na baadhi ya wananchi kuathirika, ni dhahiri kwamba Jeshi la Polisi lilishindwa kudhibiti hali hiyo.

Je, ni kwa nini Vikosi vyetu vya SMZ vinashindwa kupelekwa haraka ili kusaidiana na Jeshi la Polisi katika kuweka hali ya amani katika nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza ningependa nichukue fursa hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi na Vikosi vyetu vya SMZ kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha amani na utulivu katika nchi hii. Mhe. Spika, kama si Vikosi vya Ulinzi na Usalama hali ya Zanzibar ingekuwa nyengine leo, ni jitihada zao wanazozifanya katika kuhakikisha wanaweka utulivu wa nchi yetu na hatuna budi sote viongozi kushirikiana na vikosi hivi kuhakikisha kwamba usalama na amani katika nchi yetu unakuwepo.

Mhe. Spika, rasilimali pekee ya nchi hii ni ya amani na utulivu na maendeleo yote yanatokana na amani na utulivu. Kwa hivyo, ni wajibu wa kila kiongozi, kila mwananchi kushirikiana na vikosi vyetu hivi kuhakikisha hatua mbali mbali zinachukuliwa ili amani na utulivu uwepo. Mhe. Spika, kila linapotokea vurugu kubwa pale ambapo Jeshi la Polisi linahitaji kushirikiana na Vikosi vya SMZ hufanya hivyo na vikosi vyetu hushirikiana vizuri na tutazidi kuwafahamisha wenzetu wa polisi kwamba wanapoona tu alama ya tatizo na wao wanahitaji msaada huo basi kuhimiza vikosi vitaarifiwe mapema ili hatua zichukuliwe mapema kudhibiti hali isilete machafuko katika nchi yetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa nchi yetu katika siku za karibuni ilikuwa ikikumbwa na mambo mengi ya uvunjifu wa sheria na kutokuwa na amani na tumeona jinsi ya vikosi vyetu vinavyosaidiana na Jeshi la Polisi katika kuleta amani. Je,

serikali yake ina mikakati gani ya kuboresha Vikosi vya SMZ kwa kuvipa zana za kileo na kuwapa mafunzo ya kisayansi ya kileo katika kupambana na vurugu zinazojitokeza mara kwa mara.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri kutokana na maswali ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kwanza naomba niweke wazi kuwa, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Vikosi vya SMZ sasa ambavyo vinaitwa Idara Maalum imeundwa rasmi na kwa mujibu wa sheria tunazopitisha humu Mhe. Spika, Sheria Nam.9 ya mwaka 2010 ambazo zimeundwa rasmi kwa vikosi hivi na naomba ninukuu Katiba.

"inasema kwamba kutakuwa na Idara Maalum ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi zake na shughuli zake zitakuwa kama zilivyoidhinishwa katika sheria zinazohusika".

Sasa uchukulie sheria moja moja, kwanza Sheria Nam. 1 ya mwaka 2003 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Sheria Nam. 6 ya Mwaka 2003 ya JKU, Sheria Nam.5 ya mwaka 2004 ya KVZ na Sheria Nam. 3 ya Chuo cha Mafunzo nasema kwamba vyote vina jukumu la ulinzi na usalama wa Zanzibar. Hilo naomba lieleweke wazi na imewekwa wazi kwamba, katika sheria hizo watasaidiana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka usalama wa Zanzibar, hiyo imewekwa wazi kwenye katiba na kwenye sheria. Kwahivyo, hakuna *dispute* kuhoji kwamba kwa nini KMKM wanasaidia polisi, iko wazi kabisa kwenye sheria tumeipitisha hapa Mhe. Spika.

Vile vile serikali yetu itajitahidi kuhakikisha kwamba vyombo hivi vinakuwa na zana kamili na za kisasa na mbinu za kisasa kulinda Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Nam. 45

Baraza la Vijana

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny. Mhe. Viwe Khamis Abdalla) - Aliuliza:

Mhe. Waziri kwa kuwa Mhe. Rais wetu mpendwa aliahidi ndani ya Baraza hili tukufu wakati alipofungua rasmi kuhusu suala la Mkutano wa mwanzo wa Baraza kuundwa kwa Baraza la Vijana Zanzibar lakini mpaka leo bado. Na vijana huwa wanatuuliza mara kwa mara kuhusu uundwaji wa Baraza hilo.

Je, Mhe. Waziri ikiwa swali hili limeshaulizwa na zaidi ya watu watatu kwenye Baraza hili, lakini hatujaona mafanikio hivi utatueleza nini kuhusu Baraza hilo ambalo limeshachukua muda mkubwa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii, lakini pia naomba uniruhusu niseme maneno machache kabla sijaanza kujibu swali hili.

Leo asubuhi nilivyokuwa nasikiliza dondoo za magazeti nimesikia wanasema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaanzisha Mahkama ya Wanawake kwa ajili ya ubakaji. Mhe. Spika, nakumbuka jana mimi sikukubali kuanzisha Mahkama ya Wanawake kwa hivyo, naomba kuwaambia wanawake wasiwe na wasiwasi wowote hakuna Mahkama ya Wanawake isipokuwa Mahkama ya Watoto tayari ipo. Ahsante Mhe. Spika, sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 45 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi kuanzisha Baraza la Vijana alipozindua Baraza lako tukufu. Aidha, ni kweli Baraza la Vijana limekuwa likiulizwa sana kuhusu uanzishwaji wake hapa Zanzibar.

Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa Waraka na Rasimu ya Mswada wa Uundaji wa Baraza la Vijana Zanzíbar. Waraka na Rasimu ya Mswada wa Baraza hilo uliwasilishwa katika kikao cha Makatibu Wakuuu kwa kujadiliwa. Makatibu Wakuu baada ya kuupitia Waraka na Rasimu ya Mswada huo waliufanyia marekebisho makubwa na

walipendekeza kwa wizara kuufanyia marekebisho na kutafuta uzoefu wa nchi mbali mbali ambazo zimeshaunda Mabaraza ya Vijana.

Mapendekezo ya Makatibu Wakuu tayari yameshafanyiwa kazi. Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto baada ya kufanya mapitio ya Mabaraza ya nchi mbali mbali Baraza la Vijana la Kenya limeonekana kukidhi mahitaji ya Baraza la Vijana la Zanzíbar baada ya kufanya marekebisho kulingana na matakwa na mahitaji ya Zanzíbar. Baada ya kufanya marekebisho hayo wizara imeyapeleka tena mapendekezo hayo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mara ya Pili ili kuandaliwa Mswada wa Sheria ambao utawasilishwa tena kwa Makatibu Wakuu, Baraza la Mapinduzi na hatimae kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, lengo la serikali ni kuunda Baraza la Vijana wa Zanzíbar lenye nguvu madhubuti na lenye uwezo ambalo litaweza kutekeleza vizuri majukumu na wajibu wa kuwatumikia vijana wenzao na Taifa kwa ujumla. Hivyo kuchelewa kuundwa kwa Baraza hili ni kwa nia njema ya kutengeneza mfumo mzuri utakaoleta mafanikio kwa vijana na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwa kuwa hivi karibuni Tanzania iliridhia mkataba wa *Africa Youth Charter*, Mkataba wa Vijana wa Afrika, na kwa kuwa moja ya masharti ya mkataba huo ni nchi zilizoridhia kuwa na Mabaraza ya Vijana na tokea Mhe. Rais alipotoa kauli ya kuunda Baraza hili ni miaka mitatu sasa.

Je, kucheleweshwa kwa kuundwa Baraza la Vijana serikali haioni kwamba inawanyima fursa vijana wa Zanzibar kufaidi fursa zinazopatikana katika mkataba huo wa vijana.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, Serikali haioni kwamba imewanyima vijana haki ya kupata Baraza lao la vijana na mapema, lakini serikali imehangaika sana kuona kwamba tunafanya kitu cha maana na chenye nguvu katika nchi kwa maendeleo ya nchi yetu na vijana wetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi miongoni mwa Wajumbe wake ni vijana walio makini, na kwa kuwa serikali imetujuilisha kwamba Kenya wana Baraza la Vijana lililo zuri. Je, haoni haja ya kuwachukua Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi vijana ukawapeleka Kenya kwenda kujifunza ili wakaridhika na wao kwa niaba ya Zanzibar.
Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nadhani ikiwa Baraza letu la vijana litakuwa tayari kuanza kazi na wizara ikiwa ina mpango wa pesa kidogo tunaweza tukawapeleka vijana kwenda kuona hali ya mambo inavyoendelea kwa wenzetu.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake mama amesema kwa kuwa amechukua *sample* katika Baraza la Kenya kulingana na mazingira ya Zanzibar. Je, ni Mabaraza mangapi aliyowasiliana nayo kabla ya kwenda Kenya.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, tulipita katika nchi jirani mfano Malawi, Ethiopia, Uganda ili kutafuta habari na namna ya utaratibu wenzetu walivyoanzisha mabaraza haya. Lakini tukaona kwamba Kenya kwa nchi yetu sisi itakuwa muwafaka zaidi kuliko haya Mabaraza mengine yaliyoanzishwa katika nchi hizi.

Nam. 38

Tatizo la Udanganyifu Katika Ajira

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:

Hivi karibuni wimbi la udanganyifu wa ajira, mishahara pia viinua mgongo limezidi kuongezeka huku fedha za walipa kodi zikiendelea kupotea na bila ya hatua zozote kuchukuliwa kwa wahusika.

(a) Ni nani anayeandaa taratibu za malipo ya maslahi hayo kisheria.

(b) Ni taasisi gani kati ya Idara ya Utumishi ya Wizara husika, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo anaepaswa kubeba lawama pale panapotokea wizi au udanganyifu kama huo.

(c) Hivyo serikali huogopa nini hata kushindwa kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika na wizi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye sehemu (a), (b) na (c) na kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza sikubaliani na maelezo ya awali ya Mhe. Mwakilishi kuwa udanganyifu wa ajira, mishahara na viinua mgongo unazidi bila ya hatua kuchukuliwa kwa wahusika.

Serikali ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Dr. Ali Moh'd Shein imeunda Wizara nzima ya kusimamia masuala ya utumishi, maslahi ya watumishi na mipango kazi ya watumishi ambayo pia inasimamia Utawala Bora. Aidha, kila muhimili wa serikali una tume ya kuangalia masuala yote ya wafanyakazi yakiwemo niliyotangulia kuyataja, kwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011.

Kazi inayofanywa na wizara na vyombo vyake ndiyo iliyowezesha kubaini makosa aliyoyasikia Mhe. Mwakilishi ambayo yote yanashughulikiwa kwa kufuata sheria sahihi. Aidha, tume hizo chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma zinafanya kazi zao kwa umakini na uadilifu na hatutegemei vyombo hivyo vitaruhusu udanganyifu katika ajira.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Maandalizi ya maslahi ya Watumishi wanaostaafu yanaandaliwa na Wizara au Taasisi husika na hatua inayofuata hupelekwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa mwisho kabla ya kupelekwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo au Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa malipo. Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora huwa inapokea nakla na ombi la kuwaondoa wastaafu katika mfumo wa malipo na inafanya hivyo mara baada ya kupata taarifa sahihi.

(b) Ofisi zote zina jukumu la kupitia kazi iliyofanywa na mtu au taasisi nyengine. Linapotokea kosa huchunguzwa lilianzia wapi na lengo lilikuwa ni nini. Aidha, akipatikana aliendaa au kuanzisha udanganyifu au aliyezembea, hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yake.

(c) Kwa bahatí mbaya, wezi anaowataja Mhe. Mwakilishi na kwa maelezo yake kwamba, serikali inawaogopa mimi siwafahamu. Iwapo Mhe. Mwakilishi anawafahamu watu hao naomba anipatie tarifa zilizo sahihi ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya kitaalamu ya Mhe. Waziri naomba niulize swali la nyoingeza. Katika maelezo yake ya msingi Mhe. Waziri ya mwanzo anasema hakubaliana na maelezo yangu ya utangulizi kwamba kuna ongezeko la wimbi la udanganyifu wa ajira, viinua mgongo na mishahara. Lakini Mhe. Waziri naomba anieleweshe iwapo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watampatia orodha ya watu waliofanya udanganyifu atachukua hatua gani za haraka na muhimu sana na ataweza kuwatangazia Wawakilishi kwamba kweli kuna tatizo hili na hatua iliyochukuliwa ni hii.

Lakini pili, iwapo Mhe. Waziri amesema kwamba tume zake zimedhibiti suala hili na suala la udanganyifu limekuwa sasa ni adimu, anaweza akatwambia tatizo lililotokezea Idara ya Ujenzi la upotevu wa fedha za umma limefikia hatua gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza mimi pamoja na wizara yangu na serikali nzima kwa jumla niko tayari saa yoyote nikipewa taarifa na Baraza lako tukufu au yeyé mwenyewe binafsi kwamba wako watu ambao wamefanya makosa juu ya udanganyifu wa ajira basi tutachukua

hatua, kwani Sheria ya Utumishi wa Umma inairuhusu Kamisheni ya Utumishi wa Umma kupokea malalamiko iwapo kwamba kuna udanganyifu wa ajira umefanyika na hatimaye Kamisheni itaweza kuchukua hatua. Ikibaini kwamba udanganyifu au upendeleo au suala jengine lolote limefanyika kinyume na sheria basi Kamisheni ya Utumishi inao uwezo wa kusimamisha ajira hiyo na hatimaye kutangaza upya uajiri huo.

Swali (b) je, ninalifahamu suala lililotokezea Idara ya Ujenzi nimelisikia lakini mpaka sasa vyombo vinavyohusika na kufuatilia upotevu wa fedha vinafanya kazi hizo na litakapofika ofisini kwangu rasmi basi na mimi kama wizara au kama waziri ninayeshughulikia masuala ya utawala bora nitataka kujua hatua zipi za kisheria zimechukuliwa dhidi ya hawa ambao wamesababisha upotevu au dalili za upotevu huo.

Nam. 2

Athari ya Vurugu na Sekta ya Utalii

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza**:**
Mara baada ya uchaguzi mdogo wa Bububu uliofanyika mwaka 2012 sambamba na vurugu zilizojitokeza baada ya kile kilichosadikiwa kutekwa kwa Amiri wa Uamsho, Zanzibar hali ya amani ilikuwa tete kwa kiasi fulani.
Je, hali hii kwa kiasi gani imeathiri sekta ya utalii nchini.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na.2 kama ifuatavyo

Mhe. Spika, suala la Usalama wa nchi ni jambo muhimu sana kwa watalii wanapotaka kutembelea nchi yeyote ile. Hakika nchi yenye vurugu shughuli za utalii hudorora au kusita.

Naomba Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuwaomba sana wananchi kuwaelewa kuwa biashara ya utalii ni biashara ambayo ndio msingi wa uchumi wa Zanzibar, inahitaji utulivu wa hali ya juu. Hivyo ni muhimu kuchukua kila jitihada nchi yetu ya Zanzibar iwe tulivu na hili ni jukumu la mwananchi na mkaazi wa Zanzibar, kushababikia vurugu kwa aina yoyote ile ni kuvuga uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar baada ya kadhia hizo mbili Sekta ya Utalii imeathirika kwa kiasi Fulani, kwa watalii waliokuwepo nchini kushindwa kutembelea vivutio ambavyo viko mjini na watalii waliokuwa mjini kushindwa kufika maeneo mengine kama walivyokusudia. Aidha kwa watalii walikuwa wana nia ya kuitembelea Zanzibar kwa kipindi hicho baadhi yao walighairisha safari hizo.

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha kuwa jumla ya watalii 150,026 wameitembelea Zanzibar kwa kipindi cha Januari, 2012 hadi Novemba, 2012. Aidha katika kipindi kama hicho mwaka 2011 jumla ya watalii 153,747 waliingia nchini. Hii inaonesha kwamba mwaka huu watalii wamepungua kwa asilimia 2.5 kwa kipindi cha Januari hadi Novemba. Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kwamba miezi ya Julai, Agosti, Septemba na Novemba ndio kipindi ambacho watalii waliingia kidogo nchini kulinganisha na miezi kama hiyo kwa kipindi cha mwaka jana (2011).

Mhe. Ali Salim Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka na mimi niuulize swali moja la nyongeza.
Kwa kuwa vitendo hivi ukiachia ambavyo vimezungumzwa humu kuna vitendo ambavyo vimetokezea karibuni vya kuuliwa Mapadri wetu na tayari ma-*facebook* na vyombo vya habari vinatangaza kwamba haya ni mambo ya kigaidi.
Jee, wizara yake imejipanga vipi kutoa taaluma kwa nchi za wenzetu juu ya serikali ilivyojidhatiti na kukomesha matokeo haya.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe.Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Katika hili ni jukumu la wizara yangu kupitia Kamisheni ya Utalii mara kwa mara kutoa taaluma na kutoa taarifa sahihi kuhusiana na juhudi ambazo serikali yetu inachukua. Mara kwa mara Kamisheni ya Utalii huwa inatembelea na kushiriki katika maonesho ya kitalii ya nchi za nje na katika kipindi hicho maafisa wetu hutumia fursa hiyo kueleza hali halisi ya utalii wa Zanzibar na kwa kiasi fulani huwa tunapata mafanikio makubwa na ndio maana baada ya kushiriki huko basi idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu huwa inaongezeka.

Lakini mbali ya jitihada hizo kwa kupitia taasisi za ZATI na ZATO jitihada kubwa huwa inafanywa kutoa matangazo katika maeneo mbali mbali na kupitia mashirika yaliopo nchi za nje kueleza hali ya utalii katika nchi yetu na hali ya usalama ambayo inachukuliwa kwenye nchi yetu. Tunashukuru kwamba jitihada hizo ndizo ambazo zinazozaa matunda kuona kwamba watalii wanamiminika katika nchi yetu.

Kwa hivyo kama nilivyosema Mhe. Spika, ni jukumu la Wazanzibari wenyewe kuona kwamba kila mmoja kwa nafasi yake aliyonayo anachukua jitihada ya kuhakikisha kwamba nchi yetu imekuwa tulivu ili biashara hii iweze kuendelea vizuri na nchi yetu ipate mafanikio makubwa kiuchumi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, katika jumla ya mfululizo wa matokeo haya haya hasa yaliyotokea karibuni kabisa, kulitokea kauli iliyotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ya Jamhuri ya Muungano kwamba Zanzibar kuna ugaidi, tamko ambalo inaaminika kwamba nalo limechangia kiasi kikubwa kuwatisha watalii wasije visiwa vyetu kwa sababu unapoitangazia nchi ina ugaidi ni wazi kwamba unawafanya wawe na hofu na usalama wa maisha yao na mali zao.

Sijui Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ina kauli gani juu hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba Zanzibar kuna ugaidi na hasa kwa mnasaba wa biashara ya utalii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo yaliyotolewa mimi kama Waziri nnayeshughulikia na utalii nilifanya mkutano na waandishi wa habari na nikaeleza hali halisi ya utulivu na utengamano katika nchi yetu na kwa kiasi fulani ma-*agents* wa mashirika ya utalii waliopo ndani waliichukua kauli hiyo na ndio msingi inayotuminika.

Kwa hivyo kama kuna mtu yeyote anayesema Zanzibar kuna ugaidi, kauli hiyo sio sahihi Zanzibar ni shwari kuna mtengamano mzuri na ipo salama na jitihada ambazo serikali imechukua zinaonesha kwamba nchi yetu ipo salama, ipo shwari.
Kwa hivyo kauli hiyo ya kwamba Zanzibar kuna ugaidi si sahihi na hawezi kuchukuliwa.

Nam. 24

Ujenzi wa Jengo la Abiria Uwanja wa Ndege

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza**:**

Natoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuanzisha ujenzi wa Jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume kiliopo Unguja, ili kuondoa usumbufu wa wasafiri pamoja na kukuza hadhi ya kiwanja.

(a) Je, ujenzi wa Jengo hilo unatarajiwa kukamilika lini.
(b) Ujenzi huo unatarajiwa kugharimu kiasi gani cha fedha kutoka kwa Wahisani na Serikali.
(c) Ni matatizo gani yanayoikumba ujenzi huo na hatua gani zimechukuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye sehemu (a), (b) na (c) lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

(a) Mhe. Spika, Mradi huu unatarajiwa kumalizika mwezi Januari 2014 na umezingatia takribani huduma zote muhimu za kuhudumia abiria, ndege na mizigo ikiwemo mikonga ya kuhudumia ndege (aerobridges), msikiti n.k.

(b) Mhe. Spika, Mradi huu awali ulikadiriwa kugharimu USD 70.4 milioni ili kufanikisha upatikanaji wa vifaa na huduma muhimu katika jengo hilo.

(c) Mhe. Spika, kutokana na maelezo yangu yaliotangulia ni dhahiri kuwa kusita kwa ujenzi wa jengo la abiria kumetokana na mchakato wa usanifu wa michoro ya jengo hilo la abiria na hivyo kutoa nafasi kwa mjenzi kufanya mabadiliko ya usanifu wa ndani ya jengo kama ilivyopendekezwa na muajiri kabla ya kuruhusu hatua nyengine za ujenzi wa ndani kuendelea na hali hiyo inayotokana na mkataba wa asili wa ujenzi wa jengo hilo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Jengo lile lilijengwa kwa madhumuni ya kuleta hadhi katika kiwanja chetu cha ndege cha kimataifa ili kilingane na viwanja vyengine duniani vilivyo na hivyo kuongeza sana fedha katika nchi hii kwa njia ya usafiri wa angani.
Lakini jengo hili lilisita na baada ya kusita kuna mengi yalijitokeza. Kuna wengine walisema hiyo ramani hasa iliyokusudiwa sio iliomo katika jengo lile hivi sasa. Kuna wengine wanasema hata ile yaani kile kiwango cha lile jengo lenyewe halikufikia kama lilivyokusudiwa na kwa sababu hiyo ikawa kuna kutokukubaliana au makubaliano ya kutokubaliana baina ya serikali na hawa wahisani.
J
ee, suala hili kwa kweli lina ukweli gani na la pili hivi kusita kwa hili jengo kwa muda mrefu wote huu kulikuwa na makubaliano gani baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale waliotoa fedha zao kwa makusudi ya kujenga jengo lile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kwa pamoja kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliingia mkataba na Kampuni ya *Beijing Construction Engeneering Group* kwa msingi wa kujenga jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Zanzibar. Katika mkataba huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mjenzi huyo walichokubaliana ni kwamba mjenzi ata-*design* baadae watajenga.

Katika utaratibu kama huo jukumu la mjenzi ni ku-*design* na mjengewa yeyé atakiwa kufanya *approval*. Baada ya kwisha kujiridhisha na michoro ndio mjenzi anachukua hatua. Kilichopo hivi sasa ni kwamba mjengewa hakuridhika na michoro na usarifu unaoendelea na ndio maana ujenzi ukawa umesita. Na hatua alizochukua mjengewa ni kwamba ametafuta kampuni ya ushauri; Kampuni ya ADPI ambayo tunaamini itatushauri vizuri ili tutakapokubaliana tutakapoitisha michoro ambayo tumeletewa na mjenzi litakuwa jengo hilo litaweza kukidhi mahitaji na yale malengo yaliyokusudiwa na mjengewa.

Hadi muda huu hakukuwa na ramani wala hakukuwa na mchoro na wala hakuna viwango ambavyo vimepitwa kinyume na utaratibu na mkataba ambao tumekubaliana kati ya serikali na mjenzi.

Jibu la pili, Mhe. Spika, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kila aina jitihada kuona kwamba matatizo haya ya kiufundi yanapatiwa ufumbuzi unaostahiki ili kunusuru kufikia yale malengo yalifikiwa ya jengo hilo kukidhi mahitaji na malengo yaliyokusudiwa kujenga kiwanja cha ndege cha kimataifa kwa kuzingatia mahitaji muhimu yanayoelekeza na viwango vya kimataifa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nikamuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.
Mhe. Spika, pamoja na kadhia hii yote iliyotokea, masuala ya kiufundi, suala hili tulilizungumza sana hapa Barazani lakini jawabu zikawa hazitoshelezi. Sasa jee, hizi gharama za ziada baada ya mradi kukawia nani atakayebeba mzigo huu, ni serikali au wakandarasi au nani.

Lakini swali la pili Mhe. Spika, kuna taarifa zisizo rasmi kwamba ule uwanja lile jengo la kushukia abiria katika lile eneo lililojengwa, eneo lile halitoshelezi kwa ajili ya kutua ndege kubwa na kuna taarifa tunaambiwa huenda jengo lile likavunjwa.

Hebu tupate taarifa sahihi ya serikali. Jengo lile pale lilipo lipo sahihi au litavunjwa lisogezwe eneo jengine. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ambayo aliyoyatanguliza.

Napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.
Kwa sababu jengo limefika katika matatizo ya kiufundi na ndio maana serikali kwa kupitia wizara yetu ikaamua kumuajiri mshauri mwelekezi ambaye yeyé baada ya kupitia michoro, baada ya kupitia ujenzi ndio atakayetoa mwelekeo wa ujenzi wa jengo na nani atagharamia.

Ikiwa yeyote katika wawili atagharamia ni huyu mwelekezi ndiye atakeyetoa. Kwa sababu tunajenga jengo ambalo lina uwanja wa ndege linatakiwa lichukue viwango vya kimataifa vya uwanja wa ndege, si jengo la kawaida. Kwa hivyo sisi kupitia wizara yetu na serikali kwa jumla inajua kwamba linachelewa lakini kufanya haraka halafu kukaja kukawa haliwezi kutumika vile vile lina matatizo yake.

Kwa hivyo tunawaomba sana Wajumbe waweze kuchukua uvumilivu, mshauri ameshapatikana saini imeshatiwa na ndani ya wiki mbili ataanza kufanya kazi yake rasmi; ni Kampuni moja ya Ufaransa kama alivyoitaja Mhe. Naibu Waziri pale.

Kwa hivyo hilo suala linashughulikiwa kwa kina kabisa na yote yatajulikana katika kipindi kifupi na jibu rasmi tutalileta katika Baraza lako tukufu, hali yoyote itakayotokezea baada ya mshauri huyo mwelekezi kutoa taarifa yake.

Jengo hili lilitarajiwa liwe katika mkataba wa *design and built*; yaani u-*design* halafu ujenge. Katika hatua hiyo wizara ilitarajiwa i-*approve* zile *plan* zote ambazo anatoa yule mjenzi. Sasa kwa sababu wizara wataalamu wake ni wadogo ndio maana inawaajiri wataalamu hawa ili waweze kulingana na viwango vile vya kimataifa vya ujenzi wa jengo la abiria.

Kwa hivyo tunaomba sana vilevile wananchi kwa ujumla kwamba waone serikali inajitahidi kuona kuwa jengo lile litajengwa lakini kwa kutumia nyenzo za kitaifa ili ndege zitakapokuja ndogo na kubwa ziweze kuegesha katika jengo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa ruhusa yako…*(Makofi/Kicheko).*

(Hapa Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano alitoka nje)

Mhe. Spika: Mheshimiwa Naibu usikimbie bwana. (*Kicheko*).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Naibu anaona kazi imekwisha.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba na mimi kidogo niongezee ili Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi kwa jumla waweze kufahamu kinachoendelea.

Mhe. Spika, ni kweli serikali imesimamisha kuendelea kwa ujenzi wa jengo lile na hii ni kwa sababu tunataka jengo ambalo litakalokidhi mahitaji ya kimataifa. Tumeshawasiliana na waliotukopesha ni *Exim Bank* ya China na tayari wameshafika Zanzibar na tumeshazungumza nao juu ya matatizo tunayoyaona ambayo yaliopo ndani ya jengo lile.

Lakini sisi ni wale ambao tunaojengewa lile jengo. Ndio kwa maana kama alivyosema Mhe. Waziri tumehitaji kuweka mshauri mwelekezi ambaye ni *independent consultant* ambaye atakayeweza kutoa taarifa kamili juu ya ujenzi wa jengo lile.

Kimsingi Mhe. Spika, tuna matatizo matatu kimsingi ambayo hayo mshauri mwelekezi anatazama michoro ya wajenzi, halafu na yeyé atoe ushauri wake, halafu tufanye mazungumo na wafadhili, tufanye mazungumzo na Serikali ya China.

Kwa hivyo ninachoomba tuvute subra mshauri mwelekezi yupo, anafanya kazi zake na baada ya muda mfupi atatushauri nini tufanye juu ya jengo lile. Lakini kuna matatizo ya msingi yapo na wenzetu wamesema yanaweza kurekebishika lakini mshauri mwelekezi ndiye atakayeweza kutusaidia kama yataweza kurekebishaka au hayawezi kurekebishika.

Tayari tumeshazungumza na Serikali ya China juu ya matatizo yale, tumeshazungumza na wafadhili *Exim Bank* ya China juu ya matatizo yale, tunasubiri hiyo ripoti.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wawe wastahamilivu na kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba ripoti itakapokuwa tayari, hatua za kuchukuliwa zitakapoandaliwa tutakuja hapa Barazani kuja kuliarifu Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 8

Ukosefu wa Maji katika Shehia ya Mkunguni

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza**:**

Mamlaka ya Maji Zanzibar moja katika majukumu yake ni kuwapatia na kuwasambazia wananchi wa Unguja na Pemba maji safi na salama, lakini katika maeneo ya Sipwese, Mtomkuu na Kwamgogo vijiji vilivyomo katika shehia ya Mkunguni vinakosa maji kutokana na Mamlaka ya Maji kuyaelekeza maji Mwambe, maji ambayo wananchi wa vijiji hivyo walikuwa wakitumia.

Je, kwa nini Mamlaka ikafanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:**

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 8 kama ifuatavyo:-
Ni kweli kwamba vijiji vya Sipwese Kwamgongo na Mto Mkuu vinapata huduma ya maji kutoka katika mtandao wa maji wa Kiwani na ni kweli kwamba mtandao wa maji wa Kiwani unao upungufu wa maji kuwahudumia wananachi wanaotumia mtandao huo.

Upungufu wa maji uliopo katika mtandao huu unatokana na kukuwa kwa maeneo ya makaazi sambamba na wananchi wengi kuwa na mwamko wa kuunga huduma ya maji ndani ya majumba yao. Hali hii imepelekea kuwa na mgao wa zamu tatu za maji kwa mtandao wote. Vijiji vya Sipwese, Kwamgogo na Mto Mkuu viko katika zamu moja ya mgao wa maji huo.

Hata hivyo Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Mamlaka ya Maji imeliona tatizo hili na inatayarisha kuchimba visima viwili katika eneo la karibu na tangi la Kiwani ili kuongeza uzalishaji wa maji kwa mtandao huo na tayari eneo la kuchimba kisima hicho limeshajulikana na kazi ya kuchimba kisima zitaanza mara vifaa vya uchimbaji vitakavyokamilika.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, ningeomba pamoja na majibu ya Waziri kumuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Huu mgao wa maji katika nchi yetu si jambo geni imekuwa ni kama utaratibu. Lakini hata hivyo siku ya mgao wetu vijiji maji hayapatikani, kwanini.

Kila siku tunaambiwa leo ni zamu yenu bado maji hayaenei na mimi siamini kama maji hayatoshi, lakini ni huduma mbovu ya watendaji tu. Kwa hivyo kwa nini ikawa hayaenei hiyo siku ya zamu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Katika jibu la msingi nimejibu kwamba ZAWA ina nia na ipo tayari kuchimba visima viwili karibu na tangi la Kiwani, tangi ambalo ndilo linaloteremsha maji kupeleka Kengeja na hawa wa Sepwese na Mtomkuu ndio wanaotumia bomba hilo la Kengeja ambalo linalopeleka maji,sasa maji kwa sababu ni kidogo uchimbaji huu wa visima utasaidia sana kupunguza tatizo hilo. Hilo ni moja.

La pili namuomba Mhe. Mwakilishi awe mstahamilivu kwa sababu serikali hivi sasa imekusudia kwa kusudi kushughulikia tatizo la maji. Muda uliopita tulikuwa tukishughulikia tatizo la umeme ambalo hivi sasa tumefika hatua nzuri.

Sasa hivi mtizamo wetu ni kwenye tatizo la maji. Hata wafadhili wanajua kwamba sasa hivi Zanzibar imeelekea sana katika kupambana na tatizo la maji. Tuna mradi wa ABD ambao utajenga tangi juu ya kilima Mgagadu ambao utaongezea maji katika mtandao huu huu alioutaja Mhe. Mwakilishi na ambao utaondoa tatizo la maji katika eneo alililolitaja.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kuuliza swali...

Mhe. Spika: Hii nguo hii jana nilimuona nayo Mhe. Salma, sasa nikababaika kidogo. (*Kicheko*).

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa suala hili la maji Sipwese limekuwa ni la muda mrefu sana na kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kunatarajiwa kujengwa kisima karibu na tangi la Kiwani.

Jee, Mhe. Waziri matarajio yako haya unategemea lini kisima hicho kuchimbwa na kukamilika ili wananchi wa Kiwani kuondokana na usumbufu huu wa maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kusema kweli Mhe. Spika, hivi visima tungekuwa tayari tushavichimba hivi sasa ni bahati mbaya tu kwamba mashine yetu ya kuchimbia iliharibika na ikabidi lazima tuipeleke kwenye matengenezo.

Hivi sasa wanakamilisha matengenezo ya mashine yetu kuja kuchimba visima hivi kuja kuongezea maji. Kwa hivyo hivi sasa tupo katika hiyo *system* ya kuharakisha kwamba tunakwenda kuchimba visima hapo karibu la tangi la Kiwani.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.
Mhe. Waziri nilikisia kulikuwa kuna mpango wa watu wa Raslikhaima kutuondolea matatizo ya maji Zanzibar nzima. Jee, Mhe. Waziri mpango huo bado upo uendelevu au kama si hivyo kuna tatizo gani mpaka sasa hivi wasianze kutuondolea tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, nilivyosema katika jibu langu la nyongeza nililopita hivi sasa ni kwamba hata wafadhili wanajua kuwa sasa hivi Zanzibar wameeka mkazo katika kutatua tatizo la maji.

Sasa wapo wengi waliokuja sio Ras El Khaima peke yake, lakini tunangojea wathibitishe kama hiyo kazi wataifanya. Sisi kazi tumeshafanya maeneo tumeshayajua ni mahali gani na gani itabidi tushughulikie. Hiyo kazi tumeshaifanya tayari, isipokuwa sasa hivi tunangojea hao wathibitishe kwamba wako tayari kufanya na wataanza wapi. Kwa hivyo, hilo suala sio la Ras El Khaima peke yake ni pamoja na wafadhili wengine, mbali na hii miradi ya

ADB ambayo sasa hivi inaendelea katika maeneo mbali mbali ni kwa sababu ya kutatua tatizo la maji katika maeneo yote.

Nam. 30

Upungufu wa Vitendea kazi Maskulini

Mhe. Saleh Nassor Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Elimu bure ilikuwa ndiyo sera ya elimu iliyoasisiwa na muasisi wa Mapinduzi Matukufu ya 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiendeleza sera hiyo katika awamu mbali mbali zilizopita. Hata hivyo sera ya elimu bure lazima iende sambamba na elimu bora. Elimu bora inapatikana tu kama kutakuwa na walimu bora, vitendea kazi vya kutosha kama maabara, madeski, chaki, vitabu, mazingira mazuri ya kujisomea n.k

(a) Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu upungufu wa vitendea kazi katika skuli nyingi nchini.
(b) Kwa kuwa walimu bora ndio kichocheo kikubwa cha kupatikana kwa elimu bora, kwa nini Wizara haitoi motisha (*incentives*) kwa walimu wanaofanya vizuri.
(c) Serikali inatathmini vipi ubora wa elimu na mitaala yetu katika kuandaa upatikanaji wa wataalamu wa baadae katika kada mbali mbali nchini kama vile wahandisi, madaktari, walimu, wanasayansi n.k

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 92 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake, napenda kumuomba Mola amrejeshee afya njema Naibu Waziri wangu wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ambaye hivi sasa hali yake sio nzuri na ndio maana tokea jana hatumuoni. Basi tumuombee dua arudi kwa haraka ili aje kutusaidia kufanya kazi zetu. Baada ya utangulizi huo sasa naomba kueleza yafuatayo kabla sijajibu maswali.

Ni kweli kuwa elimu bure ilikuwa ndio sera ya elimu iliyoasisiwa na waasisi wa Mapinduzi Matukufu ya 1964 marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi leo inaitekeleza sera hiyo, pamoja na kwamba inafanya mabadiliko makubwa hivi mwaka 2006 katika kuiboresha au kuifanya iwe bora zaidi.

Mhe. Spika, tumegundua katika kuipitia sera ile kwamba tuliposema elimu bure basi pia iwe elimu iliyo bora. Mhe. Spika, tumegundua kwamba kuna kasoro za msingi ambazo zinaitatiza elimu yetu kuwa bora. Kwa mfano vitendea kazi, vitabu, walimu wenye elimu wazuri na kadhalika na kwa hivyo tumeifanyia marekebisho na tunaendelea kuifanyia marekebisho, lakini bado sera ya msingi kwamba elimu iwe bila ya malipo ipo pale pale.

Baada ya majibu hayo ya nyongeza, napenda sasa kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali yake yenye fungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

(a) Serikali inakiri kuwepo upungufu wa baadhi ya vitendea kazi kama vile madarasa, maabara, walimu bora na kadhalika. Serikali inafanya juhudi kubwa sana ya kuyapunguza au ya kuyaondosha kabisa matatizo hayo. Kwa mfano katika kupunguza matatizo hayo serikali imetenga fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka 2012/2013 katika kutengeneza madeski 3,500 kwa ajili ya wanafunzi wapatao 10,500. Madeski hayo yamo mbioni kutengenezwa na baadhi yake yameshatawanywa katika baadhi ya maskuli.

    Pia ujenzi wa skuli 21 za sekondari za kisasa unaendelea vizuri na skuli 8 zimeshafunguliwa na wanafunzi wanazitumia skuli hizo. Skuli hizo zina maabara, zina vyumba vya kompyuta, zina walimu bora na kadhalika. Kwa hivyo, juhudi ya kuiboresha elimu inachukuliwa kwa dhati kabisa.

(b) Ni kweli kuwa walimu bora ndio changamoto au ndio chanzo cha kupata elimu bora. Walimu bora tunawatafuta na hivi karibuni tunaongeza walimu 400 kwa kuajiriwa ambao wameshamaliza masomo yao

Digrii ya Kwanza, Diploma na wachache wa vyeti ambao tutawaajiri hivi karibuni. Hiyo ni kuondosha tatizo la kutokuwa na walimu wa kutosha na walio bora.

(c) Mitaala ya elimu inapitiwa kila haja inapotokea. Nina furaha kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa mitaala ya elimu ya msingi ilifanyiwa marekebisho makubwa baada ya mabadiliko ya muundo wa elimu yaliyofanywa hivi karibuni mwaka 2006. Mitaala hiyo hivi sasa inakidhi haja na itafanyiwa tena marekebisho wakati utakapofika. Tathmini ya mitaala hiyo imetoa changamoto mbali mbali, changamoto hizo ni pamoja na kuona kwamba tutalazimika kuendelea kujenga skuli mpya, kununua vitabu vya kutosha.

Hivi sasa vitabu vya kutosha vimeshanunuliwa, lakini tutaendelea kuvinunua ili kila tunapoendelea kuongeza wanafunzi na kila mwanafunzi aweze kupata kitabu chake cha kusomea. Kuendesha kambi za Sayansi na vile vile kutoa kipaumbele kwa walimu na kutoa zawadi kwa walimu wanaofanya vizuri, wanaopasisha wanafunzi wengi katika maskuli yao. Lakini hivi karibuni tumeamua kwamba sio kuwapa walimu tu zawadi, lakini pia skuli zinazofanya vizuri. Skuli inayotokea ya kwanza na ya pili na ya tatu, skuli hizi zitapewa zawadi za kuzijenga, kuzitengeneza vizuri, kuzipatia maabara na kadhalika. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe Spika, kwanza nimpongeze Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha kabisa. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri maswali madogo tu ya nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Spika, skuli zetu za Unguja na Pemba zina matatizo au mapungufu makubwa ya walimu na kwa kuwa katika bajeti iliyopita Mhe. Waziri aliahidi kwamba ataajiri walimu 700 ili kupunguza tatizo hili.

(a) Je, ni hatua gani ambazo zimekwamisha kwamba hadi leo hii walimu wale hawajaajiriwa. Hilo ni la kwanza.
(b) Kwa kuwa skuli zetu za Unguja na Pemba, zile za majengo ya zamani hata na haya ya sasa, hayana miundombinu kwa ajili ya wanafunzi walemavu, kama vile *Rampo* pamoja na yale maandishi ya kupapasa *brean* na kadhalika. Je, serikali hii ina mpango gani wa kuwaondoshea usumbufu wanafunzi hawa wenye ulemavu kusudi na wao waweze kujifunza katika mazingira mazuri.

(c) Walimu

Mhe. Spika: Hilo swali la (c) liache, twende hayo mawili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Haya.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mhe. Mwakilishi kwa maswali yake (a) na (b) ya nyongeza napenda kuyajibu kama ifuatavyo. Ni kweli katika bajeti iliyopita tuliahidi tutaajiri walimu 700 ili kuongeza au kuondosha upungufu wa walimu, au kupunguza upungufu wa walimu, sio kuondosha, lakini kupunguza.

(a) Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema tutaajiri wanafunzi 400 badala ya 700, kama sio kesho basi keshokutwa na kama sio keshokutwa basi ni wiki hii hii. Walimu 400 hawa ni wa sayansi, lakini pamoja na hawa wako wengine watasomesha masomo mengine. Idadi hii tutakapoajiri sio wa mwisho tutaendelea kuchambua na kutafuta watakaotufaa ili kuajiri kipindi kwa kipindi, mwaka hadi mwaka mpaka tupate walimu wa kutosha.

(b) Kuhusu walemavu kuwatengenezea miundombinu yao ili waweze kushiriki nao vile vile katika taaluma. Kweli skuli zetu za zamani zilikuwa hazina miundombinu hiyo, lakini hivi sasa kila skuli tunayoijenga, na tutakayoijenga itakuwa na miundombinu kamilifu, tokea ramsi ili wanafunzi wenye ulemavu waweze kupita kwa urahisi. Lakini hata katika vyoo vyao, tunatengeneza sasa vyoo kwa ajili ya wanafunzi ambao ni walemavu ili waweze kuingia katika vyoo hivyo na vigari vyao waweze kufanya haja zao kwa urahisi.

(c) Kwa hivyo, juhudi zinachukuliwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuhakikisha hatuwabagui walimu wenye ulemavu, lakini tunawaundia miundombinu ili waweze kushirikiana na wenzao waliokuwa hawana ulemavu.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama asubuhi ya leo tukiwa katika majukumu yetu. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri miongoni mwa kuboresha elimu ni kuwaboresha walimu, wakiwemo walimu wa skuli za msingi. Hivi sasa kuna malalamiko mengi ya walimu wa msingi kutokana na maslahi yao, yaani mishahara.

Je, wizara yako ina mpango gani, hasa ukizingatia kwamba walimu wa msingi mishahara yao ni duni sana. Ina mpango gani wizara yako kuiboresha mishahara ya walimu wa skuli za msingi?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, swali lake linauliza tunafanya juhudi gani za kuboresha mishahara ya walimu wa msingi. Mhe. Spika, jibu ni kwamba mwaka hadi mwaka viwango vya mishahara ya walimu, sio wa msingi tu peke yake lakini walimu wote, vinaongezwa na kupandishwa. Ingawa kutokana na ufinyu wa bajeti tuliyonayo haitoshi, lakini ni kweli kwamba mishahara inapandishwa kila bajeti inapopita, hata mwaka jana uliopita katika bajeti yetu ya mwaka 2012/2013 walimu wa msingi, wa sekondari na walimu wote wameongezewa mishahara, maposho na marupurupu mengine na tutaendelea kufanya hivyo kila uwezo utakapopatikana.

Nam. 81

Kupiga Vita Ndoa za Jinsia Moja

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa mila, silka pamoja na utamaduni wa Zanzibar hauruhusu kabisa kufanya mapenzi watu wa jinsia moja. Na kwa kuwa vitendo hivi inasadikiwa vimeshamiri katika nchi yetu.

Je, ni lini Serikali itatunga Sheria ya kukataza matendo haya pamoja na kuweka adhabu kali sana wale watakaobainika kufanya pamoja na kuendesha matendo haya maovu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa silka pamoja na utamaduni na tabia za Wazanzibari hauruhusu kabisa kufanya mapenzi ya watu wa jinsia moja. Lakini sikubaliani na Mhe. Mwakilishi kama vitendo hivi vimeshamiri sana hapa Zanzibar. Vitendo hivi vipo lakini bado havijashamiri hapa Zanzibar na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia kuviondoa vitendo hivi.

Pili, serikali kwa kuliona tatizo hili na kwa nia yake ya kutaka kuliondoa tatizo hilo, tayari imeshatunga na inaendelea kuitumia Sheria ya Adhabu kushughulikia masuala yote ya aina kama hii, ikiwemo makosa hayo ya kufanya mapenzi ya watu wa jinsia moja. Sura ya 13 ya Sheria za Zanzibar yaani (*Penal Decree No. 13*) chini ya kifungu 157 kinakataza aina yoyote ya uhusiano wa jinsia moja, iwe kwa kuoana au kwa namna nyengine yoyote, pamoja na hata kusherehekea uhusiano huo iwe ni harusi au kwa namna nyengine. Sheria hiyo imeweka adhabu kali ya kifungo cha miaka saba. Sehemu ya XV ya Sheria hiyo inayohusu makosa dhidi ya utu wa mtu yaani (*offences against morality*) inayojumuisha makosa mengi yakiwemo ubakaji, zinaa, usagaji na umalaya. Makosa hayo yote yana adhabu kali zinazofikia hata miaka 30 au kifungo cha maisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri ambayo ameyajibu kwa unyonge sana, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kabla Baraza lililopita halijaakhirishwa tulipata semina kwa wataalamu kutoka Bara ambao walikuja kutuelezea mambo ya ukimwi pale. Katika kufahamishwa tuliambiwa kwamba tatizo hili la *homosexuality* lipo, baada ya kufanya utafiti sana wataalamu walituambia kwamba inakuwa shida kufikia sifuri tatu kwa sababu majengo yanayoendesha shughuli za mapenzi ya jinsia moja Zanzibar yapo, wataalamu walituambia juzi, sikuzua katika swali langu.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba hiyo adhabu ya miaka saba ni ndogo na ili kukomesha kabisa kunahitaji adhabu kubwa zaidi ya hapo ili kuondosha hiyo *homosexuality* hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, semina hiyo na mimi nilikuwepo, na ni kweli wataalamu wale walisema makosa haya au vitendo hivi vipo. Mimi ninachosema ni kwamba vipo lakini sio kuwa vimeshamiri. Lakini zaidi suala la kifungo cha miaka saba, hiki ni kifungo ambacho wewe Mhe. Mwakilishi pamoja na Wawakilishi wengine mlikipitisha hapa na kukubaliana. Sasa kama leo mnataka kukibadilisha, mimi sina tatizo ni nyinyi Wawakilishi kusema kwamba turekebishe sheria hii badala ya miaka saba iwe miaka 40 au 20 au 30, hilo ni jukumu la Wawakilishi wenyewe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria swali dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza sikubaliani na majibu ya msingi ya Mhe. Waziri ya kusema kwamba masuala haya ya vitendo vya mapenzi ya jinsia moja hapa Zanzibar havijashamiri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri azidi kufanya utafiti ili kuthibitisha hiyo kauli yake.

Mhe. Spika, katika midahalo mbali mbali, hata juzi nilihudhuria mkutano mmoja ambao ulikuwa unatoa ripoti ya vitendo vya udhalilishaji akinamama pamoja na watoto wadogo. Mhe. Spika, tatizo sasa hivi la vitendo vya jinsia moja vimekuwa vikubwa hasa kwa kulazimisha, yaani watoto wadogo sasa hivi wamekuwa wakibakwa sana, hasa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkoa wa Kaskazini Unguja.

(a) Je, Mhe. Waziri utachukua jitihada gani ya kuhakikisha kwamba vitendo hivi vya udhalilishaji hasa watoto na ninakusudia watoto wa kiume, vinakomeshwa mara moja.

(b) Pamoja na kwamba tumepitisha sheria ya adhabu ya vitendo hivi kuanzia miaka saba, lakini Mhe. Spika, hata hao ambao wa kufungwa hicho kifungo cha miaka angalau miwili, hatujasikia mtu kahukumiwa kwa kesi za udhalilishaji watoto wadogo au mapenzi ya jinsia moja.

Je, Mhe. Waziri hatuoni kwamba pamoja na kwamba tumetengeneza sheria na tumeweka adhabu, lakini bado vyombo vya kuchukua hatua, yaani mahakama haviwatendei haki watoto wetu wanaoharibiwa?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe amechanganyisha mambo, maana yake hapa kuna ubakaji ni kosa jengine na kuna vitendo vya jinsia moja, wanaume kwa wanaume hilo ni kosa jengine. Hili la wanaume kwa wanaume kifungo chake ni miaka saba, lakini la ubakaji na ubakaji wanaingizwa hawa watoto wanaume wadogo, watoto wanawake na kadhalika. Kifungo chake kinafika hata kifungo cha miaka 30. Kwa hivyo, ni makosa mawili tofauti haya.

Kwa hivyo, tunapozungumzia suala la ubakaji ni tofauti na suala la mapenzi ya jinsia moja. Sasa kutokana na hayo bado nasema kosa hili la mapenzi ya jinsia moja hayajashamiri, kushamiri kwa Kiswahili maana yake ni kwamba yapo kila pahala. Sio kweli kwamba yameshamiri, yapo lakini sio mengi kama hivyo.

Sasa tukija katika suala la kubaka Mhe. Spika, lipo kwenye adhabu hii ambayo nimesema. Sehemu ya 15 ya sheria inayohusu masuala ya makosa dhidi ya utu wa mtu. Ni kweli makosa haya yanachukua adhabu kubwa, lakini tuna matatizo mengi. Unapomuhukumu mtu na ikiwa hukuweza kutoa ile adhabu ambayo ipo, kwanza sisi tunaruhusiwa kukata rufaa na utaona hivi karibuni tulikata rufaa kwa mtuhumiwa mmoja na kifungo kikaongezwa mpaka miaka 15.

La pili, makosa haya yana matatizo na matatizo yenyewe ni kwamba kesi inachukua siku nyingi kwa sababu ya ushahidi. Ushahidi unapatikana kwa wazee na wazee wenyewe hawataki kwenda kutoa ushahidi, mpaka uwabembeleze sana na wengine hawataki kabisa. Sasa hayo ni mambo ambayo yanatukwaza. Hivi sasa tukishirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuna kamati maalum ambayo inashughulikia mambo haya ili kuhakikisha kwamba kesi hizi za ubakaji, kwa watoto wadogo wanawake na wanaume, sio wanaume peke yao, watoto wadogo wanawake na wanaume zinachukuliwa hatua tofauti, ili kuhakikisha kwamba wabakaji hawa wanakamatwa, wanapelekwa katika mahakama na adhabu kali zinatolewa. Kwa kufanya hivyo, tunajaribu kubadilisha hata ule utaratibu wa utoaji ushahidi na utaratibu mwengine wa kuchukua ushahidi mahakamani, ili yale mambo ya *technicalities* yaweze kuondoka na tuweze kumkamata huyu anayehusika.

Uhalali wa Kisheria kwa Hatua Zinazochukuliwa na Vikosi Vya SMZ

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa).

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar ya Mwaka 2013

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza juu ya mswada huu wa ZURA. Mhe. Spika, hatua tuliyofika sasa kwenye mswada huu ni kwamba tayari mahojiano kuhusu ubora wa msingi wa mswada wangu wa sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na Mambo mengine yanayohusiana na hayo yamekwisha, na ni wakati wangu wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kutokana na majadiliano yalivyokwenda, inaonekana kwamba Waheshimiwa Wajumbe, ingawa wameonesha wako tayari kwa kiasi kikubwa kupitisha mswada huu, lakini bado wameonesha ipo haja ya kufanya semina kwa ajili ya kupata ufafanuzi zaidi wa mambo yanayohusiana na mswada huu, ili kuweza kuamua kupitisha vipengele vyake vyote katika hali ya kuridhika kabisa.

Mhe. Spika, naamini kwamba wizara yangu ipo katika nafasi nzuri ya kutoa maelezo sahihi na ya kina ya kuwaridhisha Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na Mswada huu. Lakini kama Waheshimiwa Wajumbe walivyoonesha kwamba kuna mambo muhimu na ya msingi ambayo wanahitaji kuyaelewa kabla ya kupitisha mswada huu, basi naona ni vyema kuwapatia nafasi hiyo.

Mhe. Spika, hali hiyo itasaidia kuondosha dukuduku za Waheshimiwa Wajumbe na kwa kufanya hivyo tutawaweka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuelewa mswada huu na mazingira yake kwa ajili ya kupitisha kwenye Baraza, lakini pia kwa ajili ya kuufanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa sababu hiyo basi naomba nitumie kanuni ya kifungu cha 86(1), kanuni ya Baraza, toleo la mwaka 2012 kuomba mswada huu ufikishwe kwenye Kamati. Lengo la kuufikisha mswada huu tena kwenye kamati, sio kwa sababu hasa ya kupendekeza mabadiliko, lakini ni kwa sababu ya kupata nafasi ya kushauriana kwa karibu na Waheshimiwa Wajumbe, jambo ambalo bila shaka yoyote litasaidia kuwapa Waheshimiwa Wajumbe ufafanuzi wa mswada huu ambao wameonesha kwa kauli zao kwamba wanahitaji.

Mhe. Spika, Kamati hii ambayo inashauri mswada huu upelekwe ni Kamati ya Baraza itakayojumuisha wajumbe wote, kwa sababu faida ambayo itapatikana kwa kujadiliwa tena mswada huu kwenye Kamati inahitajika kwa wajumbe wote.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba utumie mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni hii ya 86(1) kupeleka mswada huu kujadiliwa kwenye Kamati hiyo kwa muda wowote ambao kwa busara zako na kwa ufanisi wa shughuli zetu utaamua.

Mhe. Spika, baada ya wizara yangu kubadilishana mawazo na Waheshimiwa Wajumbe kwenye Kamati hiyo ndio nitaomba kurudi kwenye Baraza kwa ajili ya kufanya majumuisho ya majadiliano yaliyofanywa na Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na Mswada wangu huu wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba uamuzi wako. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, kakae kitako. Makofi yanaonesha kukubaliana na maombi ya Mhe. Waziri. Kwa hivyo, hapa hapana la kusema majadiliano jana yalionekana hivyo, kwamba ipo haja ya kueleweshana zaidi juu ya mswada huu katika semina na Mhe. Waziri anakubali hiyo.

Sasa jambo liliopo ni kuakhirisha masuala ya mswada huu katika kufanya majumuisho, ili twende kwenye kamati kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 86(1). Kwa hivyo, semina hiyo baada ya kuzungumza na Katibu nadhani tutaifanya siku ya Jumamosi na Mhe. Waziri anajitayarisha na mwanzo tulikuwa na tatizo la madukhuli. Lakini kwa kiasi fulani tumejaribu tuone kwamba madukhuli japo kidogo yawepo kwenye semina hiyo.

Kwa maana hiyo, shughuli ya mswada huu tunaiakhirisha kwa ajili ya kupata kwenye semina siku ya Jumamosi na taarifa rasmi itatolewa kwenu itakuwa saa ngapi.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo tuendelee.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika
la Bandari la Zanzibar ya mwaka 2013

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza namshukuru *Allah* kwa kutupatia uhai na uzima na taufiki ya kuweza kufika katika Baraza lako tukufu leo na kuwasilisha Mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Bandari Nam. 1 ya mwaka 1997.

Pili kabla sijaanza kuwasilisha nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwasilisha mswada huu wa marekebisho ya sheria.

Vile vile napenda nichukue nafasi hii kuwapa mkono wa taazia wananchi wote wa Jimbo la Chambani, Pemba na Tanzania kwa jumla kwa kuondokewa na Mbunge wetu Mhe. Salum Hemed kwa kifo cha ghafla na Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema na awape subra wale wote ambao wako karibu naye.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari la Zanzibar ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 1 ya mwaka 1997. Taasisi hii pamoja na mambo mengine ina jukumu la kusimamia upakizi wa mizigo inayosafirishwa kupitia Bandari za Zanzibar na upakuzi wa mizigo inayoingia nchini kupitia katika Bandari za Zanzibar.

Mhe. Spika, taasisi hii kwa mujibu wa sheria yake ina jukumu la kusimamia Bandari zote tano katika mambo yafuatayo:-

1. Kutoa huduma zinazohusiana na gati;
2. Kujenga, kusimamia, kudhibiti alama zinazoongoza usimamizi wa baharini;
3. Kujenga na kuendesha bandari mpya;
4. Kufanya shughuli za kupakia na kupakua mizigo au shehena melini;
5. Kuhifadhi mizigo hata kama mizigo hiyo itashughulikiwa au imeshashughulikiwa na shirika;
6. Kusafirisha mizigo kwa niaba ya watu wengine pahala popote duniani;
7. Kuwa wasafirishaji wa abiria na mizigo baharini au nchi kavu.

Mhe. Spika, marekebisho ya sheria hii yametokana na agizo la serikali ya kubadilisha mwaka wa fedha wa shirika ambao unaanza mwezi wa Januari hadi Disemba. Kwa hivyo, imeonekana ipo haja ya kuubadilisha mwaka wa fedha, ili uanze mwezi wa Julai hadi Juni kwa madhumuni ya kwenda sambamba na mwaka wa fedha wa serikali.

Baada ya wizara kupata agizo hilo ilikaa chini na watendaji wa Shirika la Bandari na kupitia sheria hiyo kwa lengo la kuangalia mambo mengine muhimu, ambayo nayo yangepaswa kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari lililoanzishwa kwa Sheria Nam. 1 ya mwaka 1997 kwa lugha ya kigeni *Zanzibar Port Corporation Act No. 1 of 1997*. Hivi sasa ni miaka 15 na bila ya shaka shughuli za kiutendaji zimekumbana na baadhi ya matatizo na changamoto mbali mbali zikiwemo uwezo wa watendaji (*executive power*), uwezo wa Bodi ya Wakurugenzi (*power of Board Directors)* na uwezo wa Waziri (*power of the minister*) katika ufuatiliaji na ufanisi wa shughuli za bandari.

Kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza katika kuundwa chombo chengine ambacho kinashughulikia usajili, leseni kwa vyombo vya baharini pamoja na usalama wa abiria wanaosafiri katika vyombo hivyo, yaani Mamlaka ya usafiri Baharini iliyoanzishwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2009 (*Zanzibar Maritime Authority Act No. 3 of 2009*). Hivyo, kulikuwa na haja ya marekebisho na ufafanuzi wa majukumu kati ya vyombo hivyo.

Mhe. Spika, baada ya kupitia kwa kina sheria hiyo ilionekana kuna umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria hiyo katika vifungu mbali mbali.

Lengo la kuleta mapendekezo ya kuifanyia marekebisho sheria hiyo ni kuondoa mapungufu yaliyojitokeza, ili matumizi ya sheria hiyo yaweze kukidhi haja ya usimamizi na udhibiti wa bandari za Zanzibar na kuifanya iende sambamba na wakati wa sasa.

Mhe. Spika, mswada huu unakusudia kufanya marekebisho na kuleta mabadiliko katika mambo yafuatayo:-

(i) Kufuta kifungu kilichompa uwezo Mkurugenzi Mkuu kuidhinisha matumizi ya miradi ambayo gharama zake hazizidi milioni 30, ili baadaye kifungu hicho kiweze kuwekwa katika Kanuni za Fedha kwa ajili ya kukidhi mabadiliko ya mara kwa mara.

(ii) Kufuta kifungu kilichompa uwezo Waziri kuidhinisha matumizi ya miradi ambayo gharama zake zinazidi milioni 30, ili uwezo huo ubaki wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika.

(iii) Kurekebisha mwaka wa fedha wa shirika, ili uende sambamba na mwaka wa fedha wa serikali.

(iv) Kufanya marekebisho ambayo yatatoa uwezo wa Shirika la Bandari kutoa kibali cha kuondokea bandarini kwa kushauriana na Idara ya Forodha pamoja na Mamlaka ya Usafiri Baharini.

(v) Kufanya marekebisho yatakayosaidia kudhibiti uzidishaji wa abiria na mizigo kwenye vyombo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri Baharini.

(vi) Kuhakikisha hakuna chombo chochote ambacho kitaruhusiwa kuondoka bandarini bila ya kukamilisha taratibu zote zilizowekwa, ikiwa pamoja na kupata kibali cha kuondokea bandarini.

(vii) Kuhakikisha udhibiti wa uingiaji wa watu bandarini kiholela bila ya kufuata sheria.

(viii) Kuhakikisha kwamba Kanuni za Utumishi wa Shirika zitatungwa kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2012.

(ix) Mabadiliko ya sheria hiyo pia yatampa uwezo Waziri kutunga Kanuni za Kifedha.

(x) Kuipa uwezo Bodi ya Wakurugenzi, kuteua Katibu wake wa Bodi, ili kwenda sambamba na Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza maelezo yangu haya naomba Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa maelekezo ya Baraza hili tukufu naomba niwambie kwamba nimepokea karatasi ambazo zimewekwa *table* ambayo inaonesha sheria gani kongwe iliyochukuliwa, marekebisho yaliyofanywa na lile rekebisho au sheria mpya itakayokuwa.

Kwa hivyo, hichi ni kisaidizi tunaomba Waheshimiwa wote wakitumie, ili kiweze kuwasaidia kupata ufafanuzi bila ya kupitia sheria yote kama ambavyo ilivyokuwa inatajwa hapa kwamba sheria huwa ni kubwa sana. Kutokana na hali hiyo, kuichapisha yote na kuwaletea Wajumbe ambayo nyengine haitaki kufanyiwa marekebisho inakuwa ni kikwazo katika hali zote mbili.

Kwa maana hiyo, tunaomba sana Wajumbe wote kwa zile karatasi ambazo zimegaiwa hivi sasa basi waweze kuzipitia kwa ajili ya kupata ufafanuzi ndani yake humu.

Mhe. Spika, mwisho kwa nia njema kabisa na kwa kujali maslahi ya wananchi wa nchi yetu, basi nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwamba waujadili mswada huu na kutupa mapendekezo yenye muelekeo wa kuelekea pazuri zaidi na baadaye waupitishe.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana hoja imeungwa mkono na Mhe. Waziri tunakushukuru na sasa tuanze mjadala. Nichukue fursa hii kumkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Salma Mussa Bilali (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, ifuatayo ni hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar Nam. 1 ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba sote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku uhai na kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika mkutano huu wa kumi na moja, ili kuweza kuendelea kutekeleza majukumu yetu yanayotukabili ya kuwatumikia wananchi wetu.

Pili napenda nikushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa jinsi unavyoliendesha Baraza hili tukufu kwa uadilifu na kwa umakini mkubwa, hakika hali hii inaonesha ni jinsi gani ulivyo mweledi katika kukuza demokrasia katika chombo hiki muhimu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia wakati wa kupitia na kuuchambua mswada huu.

Mwisho napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mashirikiano yao ya hali ya juu katika kuupitia na kuuchambua mswada huu, kazi ambayo imeniwezesha kusimama mbele ya Baraza hili tukufu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa niaba yao.

Mhe. Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
4. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Wazir Kheir - Katibu
8. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu

Mhe. Spika, baada ya shukrani na pongezi hizo sasa naomba uniruhusu kutekeleza azma ya kuwepo hapa ambayo ni kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar Nam.1 ya 1997 na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mswada huu unakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Kuanzishwa Shirika la Bandari la Zanzibar Nam.1 ya 1997, marekebisho ambayo yanapendekeza kuweka mazingira bora ya uendeshaji na udhibiti wa bandari. Sambamba na hayo marekebisho hayo yatapelekea kukuza uwiano na mashirikiano mazuri kati ya Shirika la Bandari na Mamlaka ya Usafiri wa Bahari.
Kamati yetu inakubaliana na dhamira hii ya serikali ya kuweka mazingira bora na uendeshaji mzuri wa bandari, kwani kila mmoja wetu anafahamu umuhimu wa bandari katika uchumi wa nchi yetu. Hivyo, kamati yetu inashauri mikakati madhubuti ichukuliwe katika kuona kwamba azma hii inafikia lengo.

Mhe. Spika, katika kuona na kuhakikisha bandari yetu inafanya kazi zake kwa ufanisi na kisheria zaidi. Kamati yetu inasisitiza kupatikana kwa wakati Kanuni za Fedha za Shirika, ni imani yetu kwamba kuwepo kwa kanuni hizi kutampa mamlaka mazuri Mkurugenzi wa Shirika juu ya uendeshaji wa shirika.

Baada ya kuupitia mswada huu Kamati yetu imependekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuuboresha mswada huu kama ifuatavyo;-

Katika kifungu cha 6(c) Kamati imependekeza kuingizwa kwa maneno " kabla ya kuondoka" baina ya neno "italazimika" na "kukamilisha" kamati imependekeza hivyo ili kukidhi tafsiri ya mswada wa kiingereza.

Vile vile katika kifungu cha 8 kamati imependekeza kwamba maneno "sheria mama" yaliopo baina ya neno "maneno" na "na" yasomeke "Sheria hii"

Mhe. Spika, Kamati yangu pia imefanya marekebisho ya uchapaji kama ambavyo yanaonekena katika waraka wangu wa marekebisho tuliouwasilisha kwako na nakala kusambazwa kwa Wajumbe. Hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuupitia waraka huo.

Kwa muhtasari hayo ndio mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar Nam. 1 ya 1997 na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Sasa kwa heshima nawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie vizuri mswada huu, kwa lengo la kuuimarisha zaidi na hatimae kuukubali bila ya pingamizi yoyote, kwani ni mswada muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kutamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja na kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuweza kutia baraka hasa kwa Mhe. Waziri aliyekuwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii na leo kuweza kututilia Fat-ha.

Kwanza na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu, Msaidizi Katibu pamoja na Wakurugenzi wake wote kwa jitihada ambazo wanajaribu kutusaidia sheria kwa ajili ya kuleta ufanisi kwenye idara zao.

Pili nimshukuru kaimu wangu Mhe. Salma Mussa Bilali hapa aliyesoma hii ripoti ni mwanafunzi mzuri amefuzu, yaani amesoma vizuri ni sawa na jana pia alisoma vizuri Mhe. Marina Joel Thomas, na hivi ndivyo inavyotakiwa taaluma Mhe. Spika, lazima tuwa-*train* kidogo kidogo kwa kuwa sisi wengine wazee tunaweza tukang'atuka. Kwa hivyo, niwashukuru sana Mhe. Spika na wala sioni tabu ukanipongeza Mwenyekiti wako kwa kuwa si mchoyo nawapa akinamama tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze kwa kuchangia na kwanza naomba sana Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu kwa sheria hii ambayo tunaiunga mkono hapa leo. Kwa kweli ni moja katika kuimarisha bandari yetu na hasa hivi sasa tumo kwenye ushindani kati ya nchi jirani za wenzetu kama vile Bara, Mombasa na nyenginezo.

Kwa kweli tuliona hali hiyo Kamati yetu, Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake na tukaona sasa iko haja kwa makusudi mswada huu uje kwa wakati wake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ametekeleza hivyo kwa kupitia Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuona kuna mambo ambayo hupitwa na wakati na lazima tuyarekebishe, ndio maana nikasema kwamba mara nyingi sana huwa sheria zetu zinapitwa na wakati na wala si vibaya tukaja kuzirekebisha, ili twende na wakati wa *technology* (*digital*) hivi sasa na tunaondoka kwenye mambo ya *analogue*.

Mhe. Spika, ripoti yetu kwanza naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Vile vile kuna mambo kwenye ripoti tuliyasisitiza hasa na tuliona kuwa hasa kutakiwa kumkubali Mkurugenzi kifungu hichi kinachompa mamlaka hivi sasa cha kuweza kutumia fedha ambazo ni kima kikubwa zaidi kuliko kile alichokuwa akitumia.

Suala hili tunakubaliana nalo na ndio maana jana nilisema kwamba jamani tukiunda hizi mamlaka au mashirika, basi tujaribu kuwaachia wenyewe wabuni mbinu wenyewe, kwa sababu wao wanao wataalamu, wanasheria pamoja na bodi zao na wote ni watu ambao ni wazuri kabisa na wanaweza kufanyakazi vizuri.

Kwa hiyo, nikasema kwamba tukubaliane nacho hichi kifungu bila ya kumpa matatizo yoyote, isipokuwa tuliweka msisitizo kwamba lazima kanuni itungwe haraka sana. Mhe. Spika, suala hili tulilisema kuwa kanuni ndio ambayo itakayompa yeye sheria au mamlaka ya kuweza kufanya yale mambo ambayo tumekubaliana.

Vile vile tulikubaliana kwamba tunayo *paper* hii ambayo tayari Mhe. Waziri ameshasema, isipokuwa na mimi nataka niwashawishi Waheshimiwa Wajumbe wenzangu. Kwa kweli humu ndimo ambapo na sisi tulipita kama Kamati na tulisema kuwa *paper* hii ambayo ipo katika hali ya kitaalamu kabisa, yaani ni wanasheria waliokutana wa Bandari pamoja na Wanasheria wa Serikali na walikaa kwa kina kabisa na tumewaamini Mhe. Spika, kuwa marekebisho ambayo watakayowaletea Wajumbe yatakuwa ni mazuri tena ni ya kisasa na yamo kwenye *technology* ya sheria.

Mhe. Spika, naomba sana wajaribu kuipitia hii *paper* ambayo yenye utaalamu wa wanasheria wawili hawa wa serikali na bandari. Kwa hivyo, sisi tulikubaliana nao vizuri na pia Waheshimiwa Wajumbe tukienda huko ndio tutafaidika zaidi na hapo ndipo mtakapoweza kutoa mawazo yenu na sisi kamati mtaweza kutusaidia, kwa sababu kamati nayo haina macho manne, isipokuwa tunayo macho mawili na nyinyi wenzetu mukiangalia na yenu mawili itakuwa ni manne na mtaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, hiyo ndio naanza msemo wangu kwa sababu kama tunavyojua hivi sasa bandari yetu. Kwa mfano, juzi sheria ilikuja kuhusu masuala ya vyombo na tukaona hivi sasa tuainishe ni jinsi gani ya abiria na mizigo na sheria hii nayo imo marekebisho yake na tumeonesha kwa jumla jumla. Kwa hiyo, hilo tumekubaliana nalo na tukasema basi hayo ni miongoni mwa mambo ambayo tumeweza kuletewa hapa, kwa ajili ya kusahihisha kwa lengo la kufahamu Waheshimiwa Wajumbe kinachoendelea zaidi.

Mhe. Spika, mswada kama unavyoonekana kwenye gazeti lenyewe ni mswada mdogo sana, lakini ni mzuri tena ni mzito sana.

Kwa kweli bandari yetu tunaielewa sote kwamba ni sehemu moja ambayo inayokuza uchumi wetu. Sasa kuna mambo ambayo yanatuwajibikia kuwa lazima tuwe na vyombo vya kisasa, hivyo ni moja katika sheria hii nayo inazingatia katika kuipa *power*, ili tuweze kuwa na vyombo vya kisasa kama wenzetu.

Mhe. Spika, bandari yetu inapendwa sana katika *East Africa*. Mhe. Spika, kwa jitihada za Mkurugenzi pamoja na watendaji wake hali halisi ya mazingira hivi sasa tutizame bandari zetu kila siku ukicha zinazidi kuwa katika hali nzuri.

Jambo jengine Mhe. Spika, juzi katika kutembea kwetu kamati kuna mfadhili mmoja alikuja akasema kwamba jamani mimi hivi sasa naomba kuwa niendeleze katika kuisaidia bandari katika utendaji huo wa kuleta ufanisi wa kujenga maofisi. Lakini bado hali hii Mhe. Spika, inanisikitisha na suala hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba watu wanajitokeza kutaka kuleta maendeleo, lakini kuna urasimu ambalo ndio tatizo letu.

Kwa mfano, tunaambiwa kati ya Katibu Mkuu wa Fedha na Mwanasheria bado hawajakaa kikato wakalimaliza suala hili. Sasa leo namwambia Mhe. Mwanasheria Mkuu na wala sina kawaida ya kumsema mwalimu wangu. Mhe. Spika, mimi nina imani labda hajapelekewa *officially* katika hali kama hii naweza kukubali hili.

Mhe. Spika, nafikiri kwamba tungeweza kukaa pamoja na hawa watu Katibu pamoja na Mwanasheria tuzidi kuimalizia ile bandari yetu na wafadhili wapo Mhe. Spika, kwa sababu huu mwanya wa *delay time* unatu-*cost*, yaani tunakosa mapato, kwani pale kila bandari ikiwa nzuri na kupata ufanisi mzuri basi na maendeleo yanapatika Mhe. Spika.

Kutokana na hali hiyo, kama hichi kitu ni kweli, basi namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika amtafute Katibu wa Fedha kwa ajili ya kulimaliza suala hili, kwa sababu hawa wawekezaji tunawakosa kwa

hii *delay*. Mhe. Spika, tunaingia umasikini na tunashindwa kuwalipa watu mishahara mizuri pamoja na kushindwa kuleta maendeleo kumbe tunajifanyisha sisi wenyewe.

Sasa hapa ninaomba sana Mhe. Spika, kwamba hivi sasa bandari inabadilisha sheria na inakwenda na wakati, lakini tuende na wakati pamoja na majengo yenyewe na sehemu zenyewe.

Mhe. Spika, nataka kumalizia ni kuwa bandari yetu ni ndogo na hili wala sioni tabu kulisema na nitaendelea kulisema kwamba bandari yetu ni ndogo na tunasema makontena 20 ya unga mbovu yaondolewe, ili ipatikane nafasi ya kuletwa bidhaa nyengine.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kupitia kwako Mhe. Spika, huyu mtu anyang'anywe leseni kuepusha kuletwa unga mbovu na wala tusione tabu, kwa sababu huko nje tunasemwa na tunaambiwa serikali ina mkono wake na mimi siamini hivyo, lakini nitaamini kwa sababu mpaka leo ni miaka mingapi anaambiwa huyu mtu aondoe, haondoi.

Nadhani ni vyema kuwaridhisha wananchi kwa sababu bandari nafasi yake ni ndogo, makontena yapo mengi na unga mbovu tunamng'ang'ania mtu kwa nini, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko namuomba kupitia kwako Mhe. Spika, amnyang'anye yule mtu mara moja au asitufanyie biashara mbovu. Kwa mfano, kuna maradhi tofauti hivi sasa kama vile vijana wanapata *cancer* na matatizo kila leo.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie hapa na naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mshimba, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadae Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuamka tukiwa hai na wazima na afya na kutupa nguvu ya kusimama hapa kuzungumzia masuala ya nchi yetu na watu wake. Nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa pili katika Mswada huu unaohusu Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar Nam. 1 ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, nisiwe mchoyo wa pongezi na shukurani, nimpongeze na kumshukuru Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa hatua yake ya kuleta Mswada huu hapa Barazani. Mswada huu ni wa pili nakumbuka Kikao kilichopita tulifanya marekebisho ya Sheria ilianzisha Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar. Pamoja na kwamba katika maelezo yake ya madhumuni na sababu na hata katika utangulizi wake, haikusema hivyo.

Mimi naamini mbali na sababu nyengine lakini vile vile ukivitizama baadhi ya vifungu vilivyorekebishwa basi Mswada huu vile vile unatekeleza mapendekezo ya zile Tume ambazo ziliundwa kuchunguza ajali mbili ambazo zilitokea mwaka juzi na mwaka jana katika visiwa vyetu. Yako maeneo unayaona kwamba yanaelekeza huko hata kama ni machache ambayo yanategemea yaongeze udhibiti na usimamizi wa masuala mazima haya ya Bandari zetu na usafiri kwa jumla.

Mhe. Spika, kabla sijaingia katika Mswada wenyewe mimi nataka nianze kwa kupongeza sana kwa kitendo cha kishujaa na kijasiri kwa kilichofanywa mwaka 1997 na serikali ya awamu ya tano ikiongozwa na Dokta Salmin Amour Juma kwa kuleta sheria hii. Ilikuwa ni kitendo cha kishujaa na kijasiri kwa sababu ukisoma Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mpaka hivi tunavyozungumza kwenye nyongeza ya kwanza mambo ya Muungano suala Nam. 11 limetajwa kwenye Bandari mambo yanayohusiana kwenye usafiri wa anga, posta, na simu.

Mhe. Spika, tukiitizama Katiba ya Muungano inatuonesha kwamba Bandari ni suala la Muungano. Lakini Bandari kwa Zanzibar ndio uhai wan chi yetu. Kwa hivyo tangu awali pamoja na kuwa imo katika Katiba ya Muungano Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuwahi haikuwahi kulitekeleza suala hili kama ni suala la Muungano.

Huko nyuma ukitizama historia kulikuwa na Shirika la Zanzibar Wharfage ambazo *legal notice* ilizozianzisha zilifutwa na sheria hii ya mwaka 1997, sheria ilianzisha Shirila la Bandari. Historia hiyo Mhe. Spika, inarudi nyuma zaidi kwa kutambua kwamba Bandari ndio uhai wa Zanzibar kama nchi ya kisiwa na kwa uchumi wetu. Nashukuru

tukitizama vijitabu ambavyo tumepewa na Wizara ya Katiba na Sheria na Afisi ya Mwanasheriia Mkuu wakishirikiana, vitabu vya *index* ya Sheria ya Zanzibar.

Mhe. Spika, tukitizama ukurasa wa 9 katika sheria kongwe ambazo zipo katika nchi yetu ni Sheria *CAP 130* inaitwa *The Port Decree* ambayo ilipitishwa tarehe 3, Oktoba, 1911 na ikafatia na sheria nyengine mbali mbali ambazo zilikuwa zinaisaidia sheria hii. Kwa sababu ya unguvu na uzuri wa sheria hii ya mwaka 1911, hata sheria hii Mhe. Spika, ya mwaka 1997 ilipokuja ilisema katika kifungu cha 71 kwamba imerekebisha au inaifuta sheria ile ya mwaka 1911 vifungu vile tu ambavyo vinapingana na sheria hii na vile vyengine vyote ambavyo bado ni vizuri na vinasaidia utekelezaje mwema wa shughuli za Bandari basi tunaitambua. Hii inaonesha histori yetu Zanzibar katika suala zila la Bandari.

Mhe. Spika, mimi nimesema nataka nianze kwa kumpongeza Rais wa awamu ya tano Mhe. Dokta Salmini Amour na aliyekuwa Waziri wake wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati huo Mhe. Dokta Amani Karume ambao ujasiri wao ulipelekea kupitisha sheria katika jambo ambalo bado mpaka hii leo Katiba hii inalitaja kwamba ni suala la Muungano. Ninachotaka kusema kama mazungumzo yangu haya ya utangulizi kwamba tukiamua tunaweza na wala hakuna wa kutuhoji wala kutubabaisha.

Mhe. Spiika, Baraza lako hili ambalo amelianzisha Rais wa Pili wa Zanzibar Mhe. Aboud Jumbe, mara nyingi Mzee wangu Mhe. Ali Mzee anapenda kulikumbusha hilo akinukuu hotuba yake awali alipokuwa akilizindua, aliita hii ni ngome ya wananchi wa Zanzibar. Sasa ngome ya wananchi ilipoamua kuwalinda wananchi ilitunga sheria hii mwaka 1997.

Mhe. Spika, natamani, ninakiu ya kuona ujasiri wa Dokta Salmini Amour akiwa Rais wa Zanzibar awamu ya tano na Mhe. Dokta Amani Karume wakati huo akiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi unaendelezwa katika Serikali ya awamu ya saba kwa kutuletea Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Mafuta Zanzibar na Sheria ya Uchimbaji Mafuta Zanzibar. Ujasiri huo ulishatangulizwa na Baraza hili mwaka 2009 ulipofanywa uwamuzi mzito, mimi nilikuwa simo lakini nawapongeza wenzangu kina Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ali Mzee, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, Mhe. Haji Omar Kheri na wengine waliokuwemo kwenye Baraza hilo, ambao waliongoza kufanya maamuzi ya kihistoria mwaka 2009 kwa kupitisha azimia, kusema suala la mafuta na gesi asilia iondolewe katika mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, hili la bandari hakuna azimio la Baraza la makusudi kusema kwamba limeliondoa. Lakini tumeamua tu kwamba uhai wa Zanzibar ni Bandari kwahiyo tunahitaji sheria hii. Sasa la mafuta Baraza hili limeamua kwa niaba ya Wananchi wa Zanzibar, lakini mpaka leo hatujapata majibu ya kuridhisha. Mhe. Spika, limelisema hili kwa sababu kwa muda mrefu tumestahamili, vikao vilivyopita tulisema kwamba serikali iwe inatuarifu kikao baada ya kikao muendelezo wa mazungumzo yanayoendelea yamefikia wapi. Kwa sababu mara ya mwisho tuliambiwa kwamba suala hili limefikia hatua nzuri na karibu tutaletewa majibu na maelezo katika Baraza hili. Namkumbusha tena Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kiongozi wa shughuli za aerikali katika Baraza la Wawakilishi na serikali inayoongoza kwa jumla tunahitaji maelezo ya serikali kuhusiana na hili na tumefikia wapi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niseme vile vile kidogo kwamba ili tufikie hapo tunahitaji ujasiri na ushupavu wa uongozi. Wananchi wa Zanzibar wanatutizama sisi na mara nyengine tunaweza kudhani kwamba hukuturidhishe au hawa tukae mbali nao tujikubishe huku kwa sababu ya maslahi fulani fulani au matamanio fulani, matokeo yake ikawa hatukubaliki kote kuwili, ikawa ndio kama wale maskini ambao wanataka kujitenga na masikini wenzao, wakajikurubisha na matajiri, wakachukiwa na wale masikini wanzao lakini wakadharauliwa vile vile na wale matajiri wanaotaka kujipendekeza kwao.

Mhe. Spika, sasa nahofia na sisi tusijetukafika pahala ikawa na sisi tukawa tunachukiwa na Wazanzibar ambao tunatakiwa kuwashughulikia katika kuwasimamia maamuzi na maslahi yao na matakwa yao wanayoyataka lakini tukadharauliwa na wale tunataka kujipendekeza kwao kwamba tuwaridhie mambo yao huku tunawakandamiza wale ambao tumewaahidi kuwatumikia. Mhe. Spika, naomba hilo niliachie hapo.

Mhe. Spika, nije katika Mswada. Mswada huu ukiutizama unaonesha kitu kimoja ambacho naomba serikali ijifunze katika hili. Sheria ya Bandari ina vifungu 71, vifungu tulivyoletewa kurekebishwa ni vifungu 7. Hii inaonesha umahiri wa utungaji sheria uliofanyika mwaka 1997, kwamba mpaka leo miaka 16 kwa wale wanaosema kwamba tuzirekebishe sheria zende na wakati, lakini tumepata vifungu 7 tu tena vya maeneo madogo sana ambavyo

vinarekebishwa. Kwa hivyo inaonesha kwamba sheria yetu tulipoitunga ilikuwa ni sheria nzuri. Nafikiri kitu muhimu cha kujifunza kwamba tunapotunga Sheria zetu tujitahidi ziwe zimekwenda mbali (zinatiza mbele) ili ziweze kufikia mahitaji ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi ninavyosema kwamba sina kubwa la kuongeza katika vifungu ambavyo vimeletwa nataka nipongeze. Moja nimefurahi katika marekebisho ya kifungu cha 30 ambacho katika Mswada huu ni kifungu cha 6 cha Mswada. Katika marekebisho yaliyofanywa kwamba imetambua Mamlaka ya Bahari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*) ambayo wakati sheria hii inatungwa mwaka 1997 ilikuwa Mamlaka hii haipo.

Lakini pili ukisoma kifungu hiki kilivyorekebishwa cha 30 ndio yale niliyosema, naomba nikisome, kwa mfano kinasema kama hivi:

> "Kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kupanga tena kifungu cha 30 kuwa 30 (1) kama ifuatavyo"

Halafu kuna maneno yameongezwa kwenye (b) aya (b) ya kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

Kifungu cha 30 (b) "Akiwa amepokea cheti kutoka kwa mfanyakazi mwenye Mamlaka ya Mamlaka ya Bahari Zanzibar kinachoeleza kwamba meli imepakia idadi ya abiria inayotakiwa tu, mabaharia imepakia vizuri na ipo katika hali nzuri kwa safari za baharini

(c) Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya aya (b) kama ifuatavyo:
Nahodha wa meli yoyote au chombo cha ndani kinachoondoka katika Bandari ya Zanzibar zilizotajwa katika jaduweli la pili ya sheria hii, italazimika kukamilisha taratibu zote kutoka katika bandari yoyote ya Zanzibar kupata cheti cha kuondoka."

Mhe. Spika, nalipongeza hilo kwa sababu kwanza moja ya mambo ambayo yametajwa katika Tume za Uchunguzi na hata wajumbe wako wengi walizungumza kwamba ni ukosefu wa utaratibu unaoeleweka juu ya nani mwenye dhamana katika vyombo wakati wa kusafiri. Sasa marekebisho haya yameondosha tatizo hili kwamba sio Ofisa tena wa Forodha. Afisa wa Forodha hahusiki na masuala haya yeye kazi yake ni kushughukia Forodha kwa hivyo ni afisa mwenye mamlaka kutoka Mamlaka ya Bahari ndiye atakayekuwa anashughulikiana na Shirika la Bandari katika kutoa *clearance* ya chombo kueleza kwamba kimetimiza masharti ili kiweze kuondokana na kufanya safari.

Ni matumaini yetu kwamba hili litasaidia kuweka usimamizi bora zaidi ili kunusuru maisha ya watu wetu ambayo yamepotea sana katika kipindi cha miaka miwili iliyopita katika ajali ambazo zimetokezea.

Mhe. Spika, langu mimi dogo tu katika hapa. Tahadhari kwa wizara kwamba tunaweza tukawa na sheria nzuri lakini usimamizi ukawa ndio tatizo kama mara nyingi ninavyosema hapa. Kwa hivyo matumaini yangu kwamba marekebisho haya yafuatiwe na usimamizi. Sasa tuone kwamba vyombo hivi tunavyoviwekea masharti haya na maofisa wao waliopewa dhamana hizi basi wanafanya kazi yao iliyokuwa imewekwa ambayo ni kuhakikisha vyombo, kwamba idada ya ibiria ndiyo inayotakikana, mabaharia wanaotakikana waliotajwa katika kanuni zao, imepakia vizuri na ipo katika hali nzuri kwa safari za baharini. Mambo haya kwamba yazingatiwe yasijeyakamalizikia katika marekebisho ya sheria tu Mhe. Spika.

Kwa sababu tunasheria ya kuona kwamba tukio likitokea tunalia sana lakini kama kawaida ya binaadamu baada ya muda tunasahau, tunarudi kule kule kwenye *biasness as usual* ambapo inaonekana kwamba ndio mtindo wa kazi pamoja na kwamba mara nyingi tunasema kwamba tunataka kuondoka hapo. Mhe. Spika, hilo kama nilivyosema nalipongeza.

Lakini jengine vile vile napongeza marekebisho ambayo yamemuondolea waziri, kwenye marekebisho ya kifungu cha 13 mbayo yametoa ruhusa kwa bodi na kwa waziri kuidhinisha kazi yoyote binafsi itakayofanywa kwa ajili ya shirika ambayo gharama zake zitazidi milioni 30 za Tanzania kama kiwango alichokuwa akikiweka mara kwa mara kuwa lazima ipate idhini yake. Sasa mamlaka haya yamarejeshwa katika bodi kwa hivyo inaonekana kwamba tunajua hasa mwenye dhamana ni nani na Waziri aliyebakia kazi zake ni kusimamia.

Mhe. Spika, hili ni zuri kwa sababu mnapowapa wote wawili dhamana halafu linapotokea tatizo la upotevu, huyu msimamizi unamkosesha nguvu ya kusimamia. Kwa hivyo nasema tunalipongeza sana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kwa jumla Mswada huu ni mzuri na maeneo aliyorekebisho yote unaona kabisa yanakubalika. Sina kubwa la kuongeza isipokuwa nilikuwa nina swali moja ambalo nitaomba hili Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho kama na Mwanasheria Mkuu atatusaidia ningeomba atusaidie.

Mhe. Spika, karibuni kumetokezea kadhia ambayo Mhe. Mshimba kaizungumza sana hapa jana, leo ya unga mbovu ulioletwa ambao unatakiwa kuondolewa. Ufahamu uliojengwa mwanzo ndio huu ambao aliokuwa anauzungumza Mhe. Mshimba kwamba aliyeleta kwa maana ya kufanya biashara ndio auondoshe. Na hili lilipelekea hata Mhe. Makamo wa kwanza wa Rais kutembelea bandari akiwa na dhamana ya mazingira na kuamuru kwamba yeye mfanyabiashara auondoe.

Lakini baadaye baada ya kufatiliwa ikaelezwa hapana kwa taratibu za kibiashara walivyokubaliana na taratibu hii sio kwa Zanzibar tu taratibu takriban kote kwenye ulimwengu wa kibiashara kamba ikiwa mimi nimenunua bidhaa au mzigo baada ya kuwa nimepokea Bandarini ndio unakuwa watu naulipia pale. Lakini madamu sijaupokea na sijaukubali mzigo unakuwa si wangu. Kwa hivyo ikaambiwa dhamana ni ya Kampuni ya Meli ilikubali kusafirisha bidhaa ambayo iko chini ya kiwango.

Ikaelezwa kwamba hii Kampuni ya Meli ambayo ina wakala wake Zanzibar ndio iwe jukumu la kubeba gharama na kuchukua kazi ya kurejesha unga ulikotoka au kwenda kuuharibu mahala pengine. Sasa inaonekana utekelezaji wa hili umekuwa mgumu, limeondoshwa hili kwenye dhamana ya mfanyabiashara na kutokana na maelezo kwamba imeridhisha kabisa kwamba mwenye dhamana hasa ni huyu msafirishaji aliyeuleta kutoka huko ulikotoka. Kwa sababu wakati anauchukua tayari ulikuwa mbovu, kwa hivyo huyu hakuupokea na hakuununua katika Bandari ya Zanzibar.

Sasa sijui kiasi gani hili linazingatiwa katika sheria zetu za Bandari kwamba yule aliyeleta chombo chake kupitia kampuni yake akaleta bidhaa ambayo mbovu Zanzibar. Je shirika la Bandari kwa kiasi gani linanguvu za kumwambia aondoshe na kumchukulia hatua badala ya kuja kuwaadhibu wale ambao hawahusiki. Nilikuwa naomba hili Mhe. Spika, tusaidiwe ili tuweze kuondosha matatizo na ufahamu ambao unawachanganya wananchi wetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nikushukuru tena na kama ulivyosema inafurahisha kuona kwamba tulifanya uwamuzi mzito na wa msingi mwaka 1997, ambao ilitupa shirika hili. Miongoni mwa wajumbe wake ambao waliweka historia ya kulianzisha katika Wajumbe wa Bodi mamo ndani ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika, tunae Mhe. Ali Mzee hapa Profesa, alikuwa mmoja katika waasisi katika Bodi ya Shirika la Bandari, tunae Mhe. Haji Omar Kheri ambaye leo ni Waziri, alikuwa ni katika waasisi katika Bodi hii, lakini pia kwa uzito wake ilikuwa na watu wazito wazito kama Shekh Abrahmani Rashid mtu mmoja maarufu sana ambaye anaheshimika sana katika nchi yetu. Ndugu Ramadhan Hilika, Captain Ramadhan Saleh, hawa wote walikuwa ni watu ambao waliianzisha Bodi ile ikiwa na watu wazito na matokeo yake wakalipa heshima Shirika hili na Zanzibar ikafanya uwamuzi wa kimapinduzi.

Zanzibar ni nchi ya kimapinduzi. Ikafanya uwamuzi wa kimapinduzi kuanzisha kitu ambacho kilikuwa kinaambiwa hakipo katika mamlaka yake na mpaka leo tunaendelea kama alivyosema Mhe. Spika, hakuna mtu aliyethubutu kuja kuhoji mamlaka ya Zanzibar nchi ya visiwa kusimamia uhai wake kupitia bandari. Kwa hivyo kama tulivyosema kwa nguvu ile ile natagemea serikali hii ya awamu ya saba itakuja kutupa jibu la uhakika kuhusu suala la mafuta na Gesi asilia tumefikia wapi, ili kama ambavyo tunapumua kwa kutumia uhai unaotokana na Bandari tuweze vile vile kusimama vizuri zaidi kwa kutumia utajiri wa rasilimali wa mafuta na gesi asilia ambayo imo katika bahari ya mipaka ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa mji mkongwe tunakutakia kila la kheria Mhe. Waziri katika marekebisho aliyeleta. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikazungumza machache kabisa katika marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari ya Zanzibar ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, kama alivyoanza Mhe. Waziri na mimi nataka nitoe pole kwa ndugu zetu wa Jimbo la Chambani kwa kuondokewa na kipenzi chao aliyekuwa Mbunge wao wa Jimbo la Chambani, tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe Makaazi yaliyomema Peponi. Amin.

Lakini vile vile nataka niwapongeze sana ndugu zetu wa madhehebu ya Katoliki au madhehebu ya Kikristo kwa kuweza kupata Papa mpya ambaye ametawazwa hivi karibuni. Tunawaombea aendelee na kazi zake na aweze kuhubiri amani katika dunia yetu.

Mhe. Spika, baada ya kutoa salamu za rambi rambi na pongezi hizo sasa naomba moja kwa moja nianze kuchangia Mswada huu na mimi kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri. Mhe. Waziri huyu wakati alipokuwepo *back bencher* mara nyingi alikuwa mkosoaji mkubwa sana hasa inapoletwa Miswada na kutokuainisha vile vifungu vya sheria au vifungu vya Mswada ambavyo vinarekebishwa. Kwa kuwa aliona kwamba sisi tutakuja kumuhoji yeye ameingia na kasi mpya na nguvu mpya na ari mpya na amekuja na marekebisho mbadala, ukiacha yale yaliyokuwemo katika huu Mswada. Kwa kweli tunampongeza sana kwa hilo.

Jengine Mhe. Spika, na mimi nataka niwapongeze viongozi wetu waliopita ambao waliasisi kuundwa kwa shirika hili. Na mimi ili iingie katika Hansard nataka nimpongeze sana Rais wetu wa awamu ya tano Mheshimiwa Dokta Salmin Amour kwa ujasiri wake wa kuweza kuanzisha hili Shirika la Bandari lakini vile vile na aliyekuwa Waziri wake ambaye pia ni Rais wa awamu ya Sita Mhe. Amani Abeid Karume ambaye alikuwa ni Waziri wake.

Mhe. Spika, shirika hili kama alivyosema mwenzangu kwa kweli limeanzishwa katika ujasiri mkubwa kwa sababu bado ukiangalia limo katika mamlaka ndani ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano. Lakini kwa kuwa shirika hili tulilianzisha kwa nia njema ya kuinua maisha ya Wazanzibari, mimi nadhani mpaka leo shirika hili linakwenda vizuri na limepita katika uongozi mbali mbali. Mwenzangu kawataja kina Mhe. Ali Mzee ambao walikuwa ndio wajumbe wa mwanzo wa bodi, kina Mhe. Ramadhani Hilika na wengineo ambao walikuwemo katika bodi ya Shirika la Bandari.

Mhe. Spika, hata na mimi niliyesimama hapa katika Bodi ya Pili ya Shirika la Bandari basi na mimi nilikuwa mjumbe katika Bodi ya Shirika hilo. Kwa kiasi fulani ndani ya wakati wetu tulifanya kazi kubwa sana chini ya Mwenyekiti wetu Mhe. Abrahamani Mwinyi Mbegu. Lakini vile vile bodi hiyo ilikuwa na Mheshimiwa ambaye sasa hivi ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Mhe. Abdalla Mwinyi vile vile na Katibu Mkuu wa sasa hivi wa Wizara ya Afya Dokta Saleh Jidawi. Hao ni baadhi ya vigogo ambao walikuwemo katika Shirika hili.

Mhe. Spika, shirika hili tangu kuanzishwa limefanya kazi kubwa sana. Mhe. Spika, tunakumbuka kwamba bandari yetu ilikuwa ipo katika hali mbaya sana na tukaweza kufanya jitihada, tukaweza kujenga bandari yetu ile ya kisasa kabisa. Lakini vile vile umahiri wa wajumbe wa Bodi wa mwanzo, gati yetu ile iliwahi kupata ajali na baadaye meli ile ikaondoka. Lakini kutokana na umahiri wa wajumbe wa bodi wakasimama kidete, wakafungua kesi Mahakama za Kimataifa na kwa kweli waliweza kushinda kesi ile na fedha zile zililipwa Shirika la Bandari na zikaweza kusaidia katika kuboresha Bandari yetu.

Mhe. Spika, Shirika hili limefanya kazi nyingi, tumeweza kuanzisha chelezo pale. Nawaomba wenzetu waliokuwepo sasa hivi, chelezo kile wakiboreshe ili kiweze kufanya kazi zaidi na kuweza kuleta tija katika hii nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo nililotaka nilizungumzie katika Mswada huu wa Sheria marekebisho nazungumza kifungu cha 11 katika hii aliyotupa kiambatanisho Mhe. Waziri, kinasema kama hivi ifuatavyo:

Kifungu cha 11 (c) “Kuidhinisha matumizi kwa ajili ya kazi yoyote ya binafsi ambayo gharama zake hazizidi shilingi milioni 30 za Kitanzania au kiasi chochote kile ambacho Shirika kinaweza kuruhusu”

Sasa huku baada ya marekebisho kwa bahati mbaya kuna *blank* haikuwekwa kitu chochote, lakini huku mwisho kabisa kinasema sababu za marekebisho kinasema kwamba kifungu hichi kimefutwa kwa hivyo ndio maana kukawa na *blank* na kimehamishiwa kwenye kanuni kwa sababu ya kuepusha marekebisho ya sheria mara kwa mara.

Sasa Mhe. Spika, hii kanuni sijakuwa na uhakika kama ipo lakini vile vile huku Waziri amepewa mamlaka ya kuweza kuunda kanuni. Sasa kama kanuni ipo basi kifungu hicho kifanyiwe marekebisho haraka haraka kiingizwe,

lakini kama kanuni haipo basi tunamuomba sana Mhe. Waziri aweze kuidhinisha kutunga hiyo kanuni ili kazi za Shirika la Bandari zisiweze kuzorota.

Mhe. Spika, nikiangalia katika mswada huu, mswada huu kwa kweli ni mdogo sana lakini pamoja na udogo wake lakini mswada huu una madhumuni makubwa sana. Na moja ambacho kitu nilichokiona nimeangalia marekebisho ya kifungu cha 13(d) kinasema kuidhinisha kazi yoyote binafsi itakayofanywa kwa ajili ya shirika ambayo gharama zake zitazidi shilingi milioni thalathini za Tanzania ama kiwango atakachokuwa akikiweka mara mara kuwa lazima kipate idhini yake. Sasa huku katika marekebisho, kuna *blank* vile vile, lakini huku mwisho kabisa kwenye sababu na marekebisho hayo kinasema nguvu hii ya kisheria alipewa Waziri na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika hivyo imefutwa na kubakishwa kwa Bodi.
Sasa hii kama alivyozungumza Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Makame Mshimba ni vizuri sasa hivi kwamba hivi vyombo tunavyovipa majukumu basi tuvipe na mamlaka ya kuweza kufanya zile kazi zao na tusiviingilie sana isipokuwa tuweze kuvisimamia. Kwa sababu kuna tatizo la kuviingilia katika utendaji wa kazi na kuvisimamia. Sasa Waziri abakie kuweza kusimamia utendaji wa majukumu haya ya Shirika.

Lakini Mhe. Spika, hapa kuna kitu kidogo nilikuwa nataka nikizungumzie. Nilitaka nikizungumzie katika kuchangia ripoti za kamati, lakini kwa kuwa tunazungumzia *specific* mswada wa marekebisho ya Shirika la Bandari naomba hiki kidogo Waziri akija anisaidie ufafanuzi, lakini vile vile nitajaribu kutoa na ushauri ambao baadae nitamsikiliza Mhe. Waziri atanijibu vipi.

Mhe. Spika, tunakubali kwamba Shirika ni mamlaka ambayo inajitegemea na inaweza kushtaki au kushtakiwa, kukopa au kukopeshwa lakini vile vile kuingia mikataba mengine ya aina yoyote katika kuboresha maslahi ya Shirika la Bandari lakini vile vile kwa watumiaji wa bandari. Hivi sasa Mhe. Spika, kuna ujenzi ambao unaendelea kufanyika katika bandari yetu ya Malindi ya Zanzibar hasa katika lile jengo la kupakia na kuteremkia abiria. Sasa hapa kidogo nilikuwa nataka nije nipate maelezo, sijui kwamba tayari tumeshakuwa na *master plan* ya ujenzi wetu wa Bandari yetu ya Zanzibar pale au ujenzi ule umefanyika ni wa *temporary* tu.

Lakini vile vile nilikuwa nataka nijue kwamba je katika ujenzi ule kuna mikataba yoyote au kuna makubaliano yoyote ya ujenzi wa ule mradi unaofanyika sasa hivi au kama ile kazi kama ni ya Shirika kuna tenda yoyote ambayo iliyotolewa na Shirika au walikubaliana tu na mjenzi katika ujenzi ule. Lakini vile vile nitataka nijue je gharama za ujenzi ule kuanzia mwanzo mpaka kukamilika kwake kwa sababu tunaona unaendelea, kwa sababu kwanza palijengwa gati pale halafu sasa hivi panajengwa mabanda ya kupumzikia abiria vile vile. Sasa nilikuwa nataka nijue je, kuna makubaliano ya aina gani ya kisheria baina ya mjenzi na Shirika ambao ujenzi ule mpaka sasa hivi unaendelea. Kama ujenzi ule ni wa mtu binafsi je, zile gharama zake atalipwa vipi na katika muda gani. Lakini je kama ujenzi ule ni wake yeye mwenyewe binafsi kama hataki kulipwa chochote, basi pia Mhe. Waziri akija ningeliomba akajaribu kunisaidia ili tukaweza kujua. Kwa sababu kama tunavyojua kwamba sisi tumewekwa hapa na wananchi na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ibara ya 5 inasema sisi tumewekwa hapa na wananchi na tutawatumikia wao. Ndio maana haya masuala wameniuliza wananchi ndio maana nikasema niyalete hapa kwa sababu hiki ndio chombo cha ukweli na uwazi.

Lakini Mhe. Spika, nilikuwa mimi nina ushauri kidogo, pale bandarini pana meli za aina nyingi zinazofunga gati. Kuna meli zile za *speed boat* ambazo hazipakii mizigo mikubwa lakini meli hizi hizi kuna nyengine mfano kama kuna *flying horse* zile zinabeba mizigo mikubwa. Sasa ile bandari kwa jinsi ilivyojengwa sasa hivi imewekwa *tiles* na zile *tiles* haziwezi kuhimili vile vigari vikubwa vya wale wabebaji wa mizigo, kwa sababu juzi Mhe. Spika, nilikiona kitu sikukifurahia sana kwamba kuna mizigo ambayo wale wachukuzi wanaibeba kutoka kule chini halafu wakishapita zile *tiles* huku ndio wanakuja kuweka kwenye vigari vyao. Sasa pale kwa kiasi fulani mimi nadhani tunazidi kuwaumiza wale wachukuzi wetu.

Sasa mimi najua kwamba huyu muwekezaji au huyu mjenzi anayejenga sasa hivi ameleta vitoroli lakini vitoroli vile haviwezi vikabeba mizigo mizito. Mhe. Spika, kulikuwa kuna mizigo pale nafikiri ya Ikulu nafikiri ilikuwa kuna tende pale, tende zile zilikuwa zipakuliwe labda kwa muda wa saa moja zilipakuliwa zaidi ya masaa matatu. Kwa sababu kwenda kubeba yaani vile vigari vinachukua uzito mdogo. Sasa mimi ushauri wangu Mhe. Spika, kwa sababu ujenzi ule haukuzingatia na watumiaji wengine umezingatia mahitaji ya mtu mmoja au ya muwekezaji mmoja, basi ni busara sikusudii kusema pavunjwe ili iwekwe njia kwa kupita yale matoroli makubwa lakini alau pangeliwekwa zulia ambavyo vile vigari vikubwa ambavyo vinabeba mizigo zaidi ya kilo 200, 300 wao alau wachukuzi wetu waweze kupita. Kwa sababu Mhe. Spika, wachukuzi wetu wale pale bandarini wakianza kukosa

kazi uko mitaani foleni zitazidi, hizi tulizokuwa nazo sasa hivi Mheshimiwa tayari kichwa kinauma. Sasa na wale wakianza kukosa kazi wataanza kuingia maungoni.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa naomba mradi kama ule unapofanyika kufanyike ile PPP ile *Public Private Patnership* na ile PPP kwa wadau wote wanatumia ile bandari. Ilikuwa pale uongozi wa Shirika la Bandari wasikilize na wachukuzi mahitaji yao lakini vile vile na wale wenye meli ambao wanaoleta mizigo yao. Sasa hivi utakuta Mhe. Spika, kutokana na ujenzi ule uliofanyika meli ya *flying horse* sasa hivi mara nyingi inafunga gati kubwa. Sasa linapokuja lile meli kubwa ile meli ya *flying horse* haiwezi kufunga kule. Lakini mimi naamini pale kama huu ushauri wangu ninaoutoa sikusudii pavunjwe lakini pakiwekwa zulia juu ya katika lile eneo ambalo ile ngazi inashuka kule chini kwenye maji ikapanda juu, ikaja zake mpaka huku chini itaweza kuwasaidia wachukuzi wetu kuweza kutubebea mizigo yetu kwa pamoja tena kwa wakati mfupi.

Sasa hili Mhe. Spika, nilikuwa ninashauri katika ujenzi ule na mimi nilikuwa natoa mchango wangu wa mawazo kwa kiasi kama hicho. Lakini vile vile Mhe. Spika, katika kuimarisha bandari yetu hivi karibuni tulipata ugeni mkubwa sana Tanzania alikuja Rais wa China Zing Ji Ping kwa bahati nzuri wenzangu baada ya kwenda China walijifundisha kichina kwa hivyo maneno hayakuwapita upande.

Mimi Mhe. Spika, mimi nilitarajia kwa sababu ugeni mkubwa kama ule halafu yule sasa hivi amekuwa nchi ya China imekuwa *investor* mkubwa katika nchi zote za Afrika na anafanya mikutano kila mwaka China kule kwa viongozi mbali mbali wa Afrika. Nilitegemea Mhe. Spika, kilio chetu cha Wazanzibari cha muda mrefu kwa kujengewa bandari yetu ya Mpiga Duri mimi nilidhania siku ile Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi wa Zanzibar Mhe. Omar Yussuf Mzee ningelitegemea pale angelisaini mkataba wa ujenzi wa bandari yetu ya Mpigaduri.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana tunashukuru tumesaidiwa miradi miwili mitatu, lakini Mheshimiwa haja yetu sasa hivi tena huo msemo wa kichina, mchina anasema anapokusaidia sio akupe samaki akupe mshipi, Mheshimiwa sisi mshipi wetu bandari ya Mpigaduri, hii miradi tuliyosaidiwa au tumepewa samaki, samaki huyu tutamla atamalizika. Lakini tungeekewa mshipi pale mimi naamini uchumi wa Zanzibar kwa kiasi fulani ungekuwa.

Sasa Mhe. Spika, labda nimuulize Mhe. Waziri labda na serikali ipo hapa tulishindwa sisi kujenga hoja, maana yake mimi naamini yule Rais alipokuwa kabla ya kuja bila shaka kulikuwa kuna vikao vya mashauriano, jamani je nyinyi mnataka nini na sisi tunataka nini tumeshindwa kujenga hoja. Mhe. Spika, mimi mara nyingi ukiangalia katika *hansard* zangu tangu nilipoingia katika Bodi ya Shirika la Bandari nilijua ni nini malengo ya bandari. Malengo ya Shirika la Bandari wamechora *right up* wakaandaa michoro kila kitu kuomba bandari ya Mpigaduri, tatizo letu tulikuwa hatuna uwezo hatujapata ufadhili mkubwa. Sasa je Mhe. Waziri mlishindwa kujenga hoja katika vikao vyenu vya pamoja katika kumkaribisha mgeni mkubwa kama yule tukajengewa angalau ile bandari yetu. Mheshimiwa bandari ile ingeweza kutusaidia sana katika kuimarisha uchumi wetu.

Sasa Mhe. Spika, na kwa sababu bandari ya Zanzibar ni bandari ya historia Zanzibar ilikuwa ndio inamiliki bandari zote za Afrika Mashariki, bandari ya Mombasa, bandari ya Mafia, bandari ya Kilwa, hata bandari ya Bagamoyo. Lakini sasa sisi bandari yetu ndio imekuwa ndogo sasa hivi kuliko hizo bandari nyengine.Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Spika, labda Mhe. Waziri aje atusaidie alau je vipi kuhusu maendeleo ya ujenzi wetu wa bandari yetu ile ya Mpigaduri.

Mhe. Spika, namalizia kwa sababu naona umeshaanza kujiweka sawa kunambia nimalizie lakini kimsingi ninashukuru kwamba katika hii sheria marekebisho itasaidia kupunguza uingizaji kiholela bandarini na sasa hivi ninashukuru pale kuna udhibiti mkubwa kabisa. Lakini vile vile Mhe. Spika, pia nilikuwa nashauri na kitu chengine bado wafanyabiashara wetu wanalalamika sana mizigo yao bandarini inachelewa. Na Mhe.Spika, tuliwahi kuzungumza uwezo wa *crane* zetu bado ni mdogo. Tunashukuru Shirika la Bandari wamenunua *crane* hivi karibuni tunaomba sana kwa kuwa hili Shirika ni Shirika linajitegemea mimi nadhani sasa hivi wangelifanya njia zao wao wenyewe kutafuta makampuni mbali mbali kutafuta nchi mbali mbali ambazo wakajaribu kushirikiana nao katika aidha kuingia ubia au kutafuta misaada ya kuboresha ile bandari yetu hasa katika kujenga zana za kuteremshia na kupakilia mizigo yetu bandarini.

Lakini la mwisho kabisa kabisa Mhe. Spika, nilikuwa naomba eneo la kuwekea makontena bado hatuna, Mhe. Spika, Shirika la Bandari mimi nadhani sasa hivi wakati umefika waanze kutafuta eneo maalum la kuwekea

makontena. Kipindi chetu sisi pale kulikuwa na eneo letu pale lipo Saateni. Lakini kutokana na mazingira ya sasa hivi eneo lile naona lishakuwa halikhalis, mimi ninafikiri pale kwa kuweka makontena ninafikiri eneo lile Shirika la Bandari basi watukabidhi tu kwa kuwa limo katika Jimbo letu la Kwamtipura eneo lile watukabidhi ili tuweze kuweka shughuli za maendeleo.

Mhe. Spika, sasa hivi tuna mambo mengi ya kuweka maendeleo katika majimbo yetu maeneo hatuna. Sasa Shirika la Bandari eneo lile lipo kwa muda mrefu mimi naomba Mhe. Waziri ninakuomba sana na nitapokuja kuchangia bajeti nitakuomba tena eneo lile Shirika watukabidhi Jimbo la Kwamtipura ili tuweze kufanya shughuli za maendeleo. Lakini kubwa zaidi nilikuwa nataka tutafute eneo la kuweka makontena ili mizigo ya wafanyabiashara isiweze kusongamana pale bandarini.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwanza nilimsahau rafiki yangu aliyekuwa Mkurugenzi wa Shirika la Bandari pale alifanya kazi kubwa sana, sasa hivi amekuwa Naibu Katibu Mkuu, tunamuombea kila la kheri katika kazi yake mpya, lakini vile vile na wale walioachiwa zile resi za kijiti basi waweze kufuata nyayo zake ili kuweza kuboresha yale maendeleo ambayo aliyoanzisha mwenzao.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache ninakushukuru ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu pamoja na udogo wake Mhe. Spika, na mimi naona si vyema angalau nipate kutoa mawazo yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu wa marekebisho ya sheria ya Shirika la Bandari, hii inaonekana haijatosha na hususan tukizingatia kutokana na majeraha au maafa yaliyojitokeza karibuni katika nchi yetu.

Pili Mhe. Spika, nichukue fursa hii adhimu kutoa pongezi zangu zaidi kwa Mkurugenzi aliyekuwepo sasa hivi ndugu yetu Captain Abdalla Juma kwa namna anavyoonesha jitihada za kusimamia sheria na kujali maslahi ya wafanyakazi wa bandari katika kipindi kifupi cha madaraka aliyopewa na Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, katika mswada mimi nitakuwa na mambo mawili madogo tu. Suala moja Mhe. Spika, liko katika ukurasa wa 340 kifungu cha 6(b) ya kifungu cha 30 cha sheria mama. Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo, kifungu cha 30 cha sheria mama kimerekebishwa kwa kupanga tena kifungu cha 30 kuwa cha 30(1) kama ifuatavyo:

a) Kwa kushauriana na Afisa wa Forodha mfanyakazi wa bandari aliyepewa mamlaka atakataa kumpa nahodha wa meli yoyote ile cha kuondokea au kuingia bandarini.

b) Aya (b) ya kifungu cha 30 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

   “Akiwa amepokea cheti kutoka kwa mfanyakazi mwenye mamlaka wa Mamlaka ya Bandari Zanzibar kinachoeleza kwamba meli imepakia idadi ya abiria inayotakiwa tu, mabaharia imepakia vizuri na ipo katika hali nzuri kwa safari za baharini”.

Mhe. Spika, hapa mimi nilikuwa na wazo pamoja na kupokea cheti kama sheria inavyoonesha mimi ninafikiri kwa maoni yangu kingeongezwa kitu ambacho kitasomeka na kujiridhisha. *Concern* yangu Mhe. Spika, kwamba suala la kupokea cheti cha kuelewa mabaharia waliokuwemo ndani peke yake hii itakuwa haijitoshelezi pasipo na kuweka kifungu cha kujiridhisha ili yule ambaye atapokea cheti kile cha kuelezea jinsi ya abiria waliopakiwa na manahodha waliokuwemo kujiridhisha ili kuona hali halisi ya meli ile kabla ya kuondoka iko katika mazingira gani.

Mhe. Spika, nazungumza hili kwa sababu *experience* inajionesha kwamba hata huko nyuma meli ambayo ilipata mitihani ya kuzama ilikuwa ina tofauti ya namna *document* zinavyoonesha abiria ambao waliokuwemo ndani ya meli na baada ya meli kuzama, pale ambapo ukaguzi ulifanywa na kubaini wale ambao waliathirika kwamba idadi inaonesha kabla ya kuzama meli idadi nyengine na takwimu ilikuwa ndogo lakini baada ya kuzama meli takwimu ikaonekana iko juu.

Sasa kwa uoni wangu Mhe. Spika, ninafikiri kuna haja ya kuongeza kitu au kuongeza maneno ya kujiridhisha ili ile *document* baada ya kuipata yule ambaye muhusika basi ajiridhishe kwanza kutokana na *document* na hali halisi ya meli ilivyo ili Mhe. Spika, hicho chombo kiweze kuruhusiwa na kuondoka bandarini. *Otherwise* Mheshimiwa hapa kidogo mimi nitakuwa nitapata mashaka tu kwamba *document* ni kwenda kwa muhusika na baada ya kupata *document* kujiridhisha na kuondoka bado sheria itakuwa haijapata nguvu na uzito kiasi hicho.

Mhe. Spika, la pili ambalo nataka kulizungumzia liko katika kifungu cha 50(a) Mhe. Spika, kinazungumza kwamba atakayeonekana katika jengo au sehemu yoyote ya Shirika bila ya kuwa na kitambulisho, ruhusa kutoka kwa mfanyakazi aliyeidhinishwa au bila ya kuwa na hati ya ruhusa au vyenginevyo. Mimi nilipongeze hili sana kwa kuleta marekebisho haya kwa kweli bandari yetu sasa hivi imekuwa ina matatizo, kuna nyakati ambazo ukifika bandarini humjui mfanyakazi, humjui papasi, humjui muuza tiketi, humjui mla unga. Sasa hili kidogo litatuondoshea usumbufu ili kwa mgeni yoyote ambaye anataka mahitaji katika eneo la bandari basi apate wepesi wa lile ambalo analihitaji ndani ya bandari na atajua nani wa kumuuliza yale mahitaji ambayo anahitaji ili kupata wepesi wa kufanyiwa shughuli zake. Ni suala jema na ni suala ambalo mimi nahisi kwamba halina mashaka.

Lakini katika eneo hili Mhe. Spika, mimi kidogo nilikuwa nataka nilizungumze suala dogo ambalo bado tunalipigia kelele wananchi wengi katika masuala ya vitambulisho kwa wale ambao wanakwenda kukata tiketi. Mhe. Spika, sijaiangalia haraka haraka sheria inasemaje kwa wale abiria ambao wanakwenda kukata tiketi kwa ajili ya safari wanapotakiwa kwenda na vitambulisho vinavyowathibitisha kwao kwamba huyu ni mtu fulani anasafiri kwa ajili ya kwenda maeneo mengine.

Mhe. Spika, tatizo ambalo nataka kulielezea kwamba kuna baadhi ya wananchi wetu wengine wanakuwa na mapungufu au wanakuwa na ukosefu wa kuwa na vitambulisho vya kuweza kukata tiketi. Sasa umetokezea utamaduni wa watu kupewa barua za masheha kama ni kitambulisho au uthibitisho wa kumthibitisha yeye kwamba huyu ndio fulani ili aweze kukata tiketi. Lakini kadhia ambayo inajionesha kwa hapa Zanzibar Mhe. Spika, unaweza *document* ile ya Sheha ukaitumia katika utaratibu mzuri. Watu wetu wa Zanzibar wanaitambua na wanaielewa na mtu anakatiwa tiketi na anaondoka. Lakini kadhia inaonekana ni pale yule mwananchi anapotaka kurejea Zanzibar kutumia ile *document* ya Sheha kwenda kukatia tiketi kule katika bandari ya Dar es Salaam, kumekuwa na matatizo makubwa Mhe. Spika. Wanachozungumza wao kwamba barua ya Sheha imeelezea jina lakini hakuna picha ya mtu ambaye inamuonesha huyu ndiye muhusika mwenyewe.

Sasa kuna baadhi ya watu wanashindwa kurudi kutokana na mapungufu hayo, huku Zanzibar barua imemuhalalishia au imemkubalia kusafiri, amepewa tiketi amesafiri. Lakini anataka kurudi Zanzibar anaambiwa *okay* hii barua inazungumza wewe ndiye Ali Salum Haji lakini mbona sura hatuioni ili kuthibitisha kama wewe ndiye Ali Salum Haji kwa mujibu wa barua uliyokuwa nayo. Mimi nafikiri kutokana sasa hivi wakati tumeletewa mswada huu wa sheria nafikiri kulikuwa kuna haja tosha na hili nalo kuliona ili kulifanyia marekebisho ili sheria kuona namna gani tunaliweka endapo ikiwa mwananchi atakuwa labda hana *document* au hana kitambulisho husika basi tueleze katika sheria yetu kwamba barua ya Sheha itatosheleza kuwa ni *document* ambayo itamthibitisha na pia ielezee kama inawezekana ikawa na picha au haina picha.

Sasa Mhe. Spika, ilikuwa hili langu nilizungumze dogo tu, na kama nilivyozungumza awali kwamba mswada huu kwa bahati ni mdogo sana lakini na mimi nikaona nitoe maoni yangu katika kutoa mchango wangu na mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono mswada huu. Mhe. Ahsante ninakushukuru.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniruhusu angalau kusema maneno mawili matatu katika mswada huu wa marekebisho ya sheria ya bandari. Kwanza kabisa Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, na anaendelea kutupa neema yake ya uhai na uzima kwa sababu bila ya hayo mawili tusingeweza leo kusimama hapa tukaweza kusema chochote.

Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, lakini tatu Mhe. Spika, nataka nimpongeze Waziri wa Miundombinu tuliwahi kusema huko nyuma kwamba sheria hizi za marekebisho zinakuwa kazi kidogo kuzizingatia kwa sababu tunakuwa hatuna ile sheria ya msingi sheria mama. Sasa tukasema kwamba basi marekebisho yaoneshe kile kifungu kama kilivyo zamani na sasa hivi kinavyotakiwa kiwe. Kwa bahati nzuri Waziri kachukua hatua za haraka haraka kutuletea na kwa kweli baada ya kutuletea hii imetupa mwanga mkubwa wa kuweza kutoa michango yetu katika marekebisho haya.

Naomba pia na Mawaziri wengine wachukue mfano wa Waziri huyu ili kufanya kitu kizuri zaidi. Mhe. Spika, haya marekebisho ni madogo sana kwa kweli kwa hivyo michango nayo haitokuwa mikubwa. Lakini ukiyazingatia ni marekebisho ya maana sana.

Mhe. Spika, mimi nianze marekebisho ya kifungu cha 30 (b) ambayo humu yametajwa kama ni marekebisho ya 6. Mhe. Spika, marekebisho haya au kifungu hiki hivi kilivyokaa sasa kimeleta ufafanuzi mzuri zaidi wa namna ya utekelezaji wa meli zetu za abiria na mizigo.

Mhe. Spika, hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia majanga makubwa ya ajali. Sasa mimi naamini moja katika madhumuni ya marekebisho haya ni kujaribu kuondoa zile kasoro kasoro ndogo zilizokuwepo ili udhibiti sasa wa upakizi wa abiria na mizigo uweze kukaa vizuri ili watu wetu wapate hali ya usalama zaidi.

Mhe. Spika, kifungu hiki ni kizuri sana na kama kawaida yetu ni mahodari kweli kweli wa kutunga sheria nzuri kama zingekuwa zinafuatwa kama zilivyo mimi nadhani nchi hii ingekuwa mfano duniani. Lakini tunapata tatizo la kwamba sheria zipo lakini hazifuatwi zipasavyo.

Mhe. Spika, pale bandarini sasa hivi ni vurugu tupu, kuna vibanda pale vilipewa leseni na kampuni za kuuzia tiketi pale na nani lakini uwe na bahati nzuri sana mpaka uweze kwenda pale kwenye kile kibanda upewe tiketi iliyo halali pale. Wale vijana wanaouza watoto wadogo wadogo wale wanachukua tiketi wanawapa wale madalali sijui nani wale, ukienda kibandani tiketi hakuna lakini dalali kakaa pembeni akishakuona umeshindwa pale anakwambia njoo mimi tiketi ninayo anakuuzia kwa bei ya juu. Halafu wanarudi huko wanakwenda kugawana pesa na wale wale watu wa kampuni zile.

Tatizo hili Mhe. Spika, tumelisemea sana lakini bahati mbaya mpaka leo watu wetu wanapata usumbufu hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kuwakomesha wale watu. Kwa nini Kampuni haiuzi tiketi zikimaliza ikawa basi mpaka wapitie njia za pembeni za kujiongezea mapato yasiyokuwa halali. Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri hili suala naomba sana ulichukulie hatua madhubuti, kama tiketi hakuna basi tusiione mkononi ukiuza.

Halafu tatizo la Pili Mhe. Spika, hii sheria hata kama sasa hivi imekaa vizuri zaidi lakini hata hapa kabla basi kama ilikuwa kuna utekelezaji mzuri basi ilikuwa haijawa na kasoro kubwa. Lakini tunapata tatizo kwamba watu wetu wa kusimamia hii sheria wale waliopewa mamlaka ya kuitekeleza hii sheria pale bandarini na wao si waaminifu kabisa. Kwa sababu unaweza ukafika pahali tiketi zote zimeuzwa abiria wameshaingia melini lakini ukatokea wewe unataka kusafiri bahati mbaya umepata taarifa pengine labda umepata msiba huko au kuna mtu anaumwa sana ukaona labda ufanye safari ya *emergency* kabisa, unakwenda bandarini tiketi hakuna vibandani lakini kuna mtu atakwambia usijali wewe utasafiri. Anapokea pesa zako halafu anakufanyia maarifa unasafiri hivi hivi kiholela holela, mtu wangu huyo! Mtu wangu huyo! anapita mle.

Sasa Wale ukiwatizama kwa upande mwengine wanamsaidia yule mtu aliye na *emergency* lakini wanasaidia sana kuikiuka hii sheria. Matokeo yake siku zote meli itakuwa na watu wengi kuliko wale ambao imepangiwa. Sasa sijui Mhe. Waziri atatumia utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba watu waliokuwa kwenye meli ni wale ambao wametakiwa kwa mujibu wa sheria na leseni aliyopewa yule mtu.

Mhe. Spika, unajua tatizo letu Wazanzibari tuna uammi mwingi, muhali mwingi, na kwa sababu ya muhali huu ndio maana hatuwezi kutekeleza sheria zetu tulizojipangia na hata mtu akivunja sheria hawezi kuadhibiwa kwa sababu ni mtu wa fulani, haya matatizo kama hatukuyaweka kando maisha Wazanzibari hatutaendelea, nilikuwa naomba sana kama tunatunga sheria basi tuondoe muhali tusimamie sheria na jamii ikishazowea kwamba sheria ikishatungwa kuwa inasimamiwa mimi nadhani ule uammi utaondoka. Kwa sababu mambo mengine Mhe. Spika, ukijaribu kukwepa sheria ukafuata uammi utaharibikiwa tu, utapata maafa makubwa na ndio haya yanayotukuta kila siku. Kwa hivyo, naomba sana uammi uammi hu bora tuuweke kando kwana.

Sayyidna Omar alikuja akaambiwa maneno ya uongo wakati yeye ni Khalifa, aliambiwa kwamba mwanawe wa kumzaa kafanya tendo la zinaa. Sasa akaona mimi ni Khalifa huyu ni mwanangu lakini kama sikumpiga mawe basi itakuwa mimi sikufuata sheria, akamuadhibu mwanawe kwa mawe na halafu ikaja ikabainika kumbe alikuwa ni mnafiki alikwenda kumwambia uongo kumjaribu lakini alitekeleza sheria. Sasa leo inakuwaje mtu aa yule mtoto wa fulani usimchukulie hatua na hivi hatuendelei mtadanganyana bure hapa, mtatumia pesa za watu bure tukitunga sheria halafu tukiziweka kwenye makabati lakini hakuna *implementation*.

Mhe. Spika, nalisemea hilo kwa nguvu kwa sababu ya matatizo tunayoyapata kila kona ya nchi yetu, kila taasisi ya nchi yetu tunapata matatizo kwa sababu ya kutokufuata sheria au kuyafuta kwa sababu ya uammi tulionao Wazanzibari.

Mhe. Spika, labda niendelee kidogo lakini nafikiri litakuwa la mwisho kwa sababu mswada wenyewe hauna mambo mengi na kwa kweli haya yaliyomo yamekaa sawa. Naomba kidogo marekebisho haya ya kifungu cha 30(2) labda nikisome hiki kifungu kidogo, tatizo langu hapa ni lugha tu basi. Inaonekana hawa waliouandika huu mswada labda wali-*translate* neno kwa neno kutoka Lugha ya Kiingereza wakati humu. Sasa mara nyengine kama ukijaribu kutafsiri neno kwa neno basi unaweza kuandika lugha isiyo nzuri. Mimi nadhani vizuri kuangalia *concept* ya ile *section* ambayo unai-*translate*.

Sasa hapa lugha iliyotumika inatutia aibu sisi Waswahili tukiandika lugha kama hii, manaake sisi Waswahili tulipaswa tuandike lugha nzuri zaidi, ingekuwa mswada umeandikwa na Waingereza tungesema hawana tatizo kwa sababu wao si lugha yao wanaigaiga tu, lakini sisi lugha yetu Mhe. Spika, hii.

Kifungu cha 30(2) kinasema kwamba:

> "Nahodha wa Meli yoyote au chombo cha ndani kinachoondoka katika bandari za Zanzibar zilizotajwa katika jadweli la pili ya sheria hii",

Kwanza hiyo ya sheria hii haipaswi kuwepo hapo iwe la sheria hii itakayowekwa. Halafu 'italazimika' hapa haitakuwa italazimika lakini itakuwa atalazimika mana tunamzungumza yule nahodha, 'kukamilisha taratibu zote kutoka katika bandari yoyote ya Zanzibar' na hii bandari yoyote ya Zanzibar ni *repetition* haikutakiwa tena hapa kwa sababu nyuma tumeshaitaja.

Sasa mimi nina *proposal* nilikuwa naomba kama waziri ataona inafaa basi hiki kifungu kisomeke kama hivi: "Nahodha wa meli yoyote au chombo cha ndani kinachoondoka kutoka katika Bandari za Zanzibar zilizotajwa katika Jadweli la Pili la sheria hii atalazimika kukamilisha taratibu zote kutoka katika Bandari hizo nakupata cheti cha kuondoka". Naomba ikiwa Waziri atakubaliana na mimi basi hiki kifungu afadhali kisomeke hivi kuliko hivi kilivyo kina matatizo ya kilugha.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache sana mimi naunga mkono mswada huu wa marekebisho kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua fursa hii na mimi kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii na nitoe mchango wangu mfupi sana kwenye mswada huu mswada ambao ni mfupi lakini una umuhimu sana.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwenye sababu na madhumuni. Mhe. Waziri kama nimemfahamu vyema amesema kwamba sababu kubwa ya mswada huu ni tatu na moja ni kuweka mazingira bora ya uendeshaji na udhibiti wa ndani, pili kukuza uiyano na mashirikiano kati ya ZMA na Shirika la Bandari na tatu kurekebisha mwaka wa fedha. Kama hizo ni sababu za msingi ambazo zimetolewa mimi binafsi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani naunga mkono hizo sababu ni za msingi na nichukue fursa hii kuwapongeza Mhe. Waziri na wizara yake kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kuleta sababu hizi na kwamba tufanye marekebisho ili sheria hii iende sambamba na matakwa ya dunia ya leo.
Mhe. Spika, sasa kutokana na sababu hizo niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 11 ambacho kifungu cha 11 cha asili kilikuwa kuidhinisha matumizi kwa ajili ya kazi yoyote ya binafsi ambayo gharama zake hazizidi shilingi milioni thalathini za Tanzania au kiasi chochote kile ambacho shirika linaweza kuruhusu. Kwa mujibu wa marekebisho haya Mhe. Spika, sasa kifungu hiki kimefutwa na kitabakishwa kwenye kanuni.

Mhe. Spika, nadhani madhumuni ya kufutwa kifungu hiki sio mabaya lakini naomba nitoe tahadhari kwamba isije ikawa ni mwanya sasa, kauli zetu zikatoa mwanya ya kuwaruhusu watendaji kutumia mwanya huo kutumia matumizi mabaya ya fedha. Kwa mfano, palikuwa na kifungu hiki tangu zamani lakini tumeshuhudia Shirika la Bandari likitengeneza Meli ya MV. Jitihada kwa shilingi 1.4 bilioni na wakati *value for money* haikuligana kabisa na matengenezo waliyofanya. Tumeshuhudia Shirika la Bandari likinunua *crane* ambayo ingekusudiwa kuchukua mizigo tani 75 lakini kuna taarifa kwamba *crane* hiyo haina uwezo huo, tumeshughuli mambo mbali mbali kwenye

shirika la Bandari. Sasa ilikuwepo sheria hii lakini mambo hayo yalifanywa, leo kifungu kinafutwa na inabakishwa kwenye kanuni.

Mhe. Spika, nadhani nitoe tahadhari kwamba isije ikawa ni mwanya wa kutoa kwa watendaji kutumia fedha za umma vibaya. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapotunga kanuni yake ikawa matakwa ya kifungu hiki nadhani wangekuwa makini sana kudhibiti watendaji wasio waaminifu kuja kutumia feda za umma visivyohalali.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho ningechangia ni kifungu cha 23 ambacho mswada huu umekusudia kurekebisha mwaka wa fedha, mwaka wa fedha wa Shirika la Bandari ulikuwa ni Januari – Disemba, kwa kweli ulikuwa unaipa tabu serikali hasa Ofisi ya CAG haiendi sambamba na ukaguzi wa hesabu za serikali katika mfumo mzima wa serikali. sasa leo kuamua kwamba wa fedha uwe ni mwaka wa Julai – Juni nadhani ni busara sana kuwa Shirika la Bandari kufuata mwaka wa fedha huo utasaidia kuweka kumbukumbu vizuri katika Ofisi ya CAG lakini vile vile utasaidia hata kamati yetu ya PAC kwenda sambamba na ukaguzi wa hesabu za serikali katika mashirika mbali mbali. Nadhani ni busara kubwa kwa wizara kuamua kurekebisha kifungu hiki ili wende sambamba na mwaka wa fedha wa serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, kifungu chengine ni kifungu cha 50 ambacho ni udhibiti wa uingiaji wa watu Bandarini bila ya kufuata taratibu zilizowekwa. Mhe. Spika, mimi nipongeze kama Mhe. Abdalla Juma alivyosema hivi leo bandarini kumekuwa na vurugu kubwa, huelewi mfanyakazi, humuelewi abiria, huelewi watu wengine kwa kweli imekuwa ni vurugu. Hivi karibuni nimekwenda Bandarini nimeshangazwa kidogo nimeona hata bandarini kunauzwa madafu, hii bandari ya meli kubwa za Serengeti na Maendeleo. Nimeshuhudia pale matenga ya madafu yanauzwa nikasema hee, Mkurugenzi mpya sasa anapanua wigo wa kibiashara mpaka madafu yanauzwa ndani ya bandari. Sasa leo kuja kwa sheria hii nadhani ni jambo la busara kwamba tuweke sehemu za biashara mbali na suala la bandari mbali, lakini kuweka madafu ndani ya bandari si jambo la busara.

Lakini Mhe. Spika, nitoe tahadhari vile vile isije tukapata mwanya wa kuwanyanyasa watu wetu, isijekuwa pia tunaondosha madafu lakini tukapata mwanya wa kuwanyanyasa watu wetu, nadhani sheria ifuatwe na tuzingatie sana umuhimu wa bandari, tuzingatie sana umuhimu wa watu wetu na taratibu za kisheria zifuatwe.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba kadiri ya mswada huu ulivyorekebishwa mimi niunge mkono kwamba napongeza katika maeneo yote yaliyorekebishwa. Lakini Mhe. Waziri nimuombe anieleze sasa, kwa sababu marekebisho ya sheria ya bandari yangekwenda sambamba iwapo bandari yetu ingepata yale malengo ya upanuzi. Tumepata taarifa kwamba kuna mfadhili alikuja nchi ya Australia kutaka kuipanua Bandari yetu ya Malindi hadi Mpigaduri, lakini kuna taarifa kwamba ufadhili ule umekwama kwa sababu kuna Katibu Mkuu amezuia ujenzi wa bandari ile. Sasa hii ni habari njema kama imekuja lakini si nzuri kama inazushwa. Sasa Mhe. Waziri nadhani kupitia Baraza hili nakupitia mchango wangu huu basi utuelimishe je huyo mfadhili alikuja kweli na ni nani aliyezuia ufadhili huu kwa ajili ya kupanua bandari yetu kwa maslahi ya wafanyakazi wetu na Wazanziabri wetu kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia angalau mawili matatu katika sheria yetu hii ya kuanzishwa kwa Shirika la Bandari. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuleta sheria hii mbele ya Baraza lako tukufu ambapo hili ni jukumu letu sisi kama Wawakilishi wa wananchi wa Baraza lako hili kupitisha sheria mbali mbali na pia zile zilizopitwa na wakati kuzifuta.
Mhe. Spika, kwanza niende na madhumuni na sababu ya mswada huu ni marekebisho ya kuweka mazingira bora ya uendeshaji na udhibiti wa bandari.

Mhe. Spika, kwenye hili mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Pia marekebisho haya Mhe. Spika, ni marekebisho yanapendekeza kukuza uiyano, mashirikiano mazuri kati ya shirika na mamlaka ya usafiri wa bahari na kuhakikisha udhibiti na uendeshaji bora wa bandari ya Zanzibar.
Mhe. Spika, kwa kweli nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kuleta sheria hii na baada ya matatizo mengi ambayo tumeyapata ya kuzama kwa meli karibu mara mbili, kwa hivyo siku zote penye shida basi na baraka au mafanikio hupatikana, siku zote penye shida basi ujue kwamba na barka pale zinapatikana na matatizo mengi yanayotukuta basi tuwe wastahamilivu na kuomba subira kwa wingi.

Mhe. Spika, kwanza mswada huu una sehemu mbili ambapo Sehemu ya Kwanza ni ile inayoelezea jina na sehemu ya pili ni marekebisho ya vifungu na sehemu hiyo ya pili ya mswada huu inapendekeza kurekebisha vifungu mbali mbali. Pia na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani nasema kwamba nakubaliana na marekebisho ya vifungu hivyo.

Lakini vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweka bayana mwaka wa fedha wa Shirika ambao utaanza mwezi wa Julai na kumalizia tarehe 30 Juni kwa kila mwaka. Kwani mashirika mengi huwa kidogo kunakuwa na mgongano mara nyingi mwaka wa fedha huwa unaanzia Januari – Disemba, kwa hivyo, nipongeze.

Vile vile nitoe mchango wangu kidogo kwa suala la fedha kwamba hapa Mhe. Waziri hajatuonesha kwamba fedha hizi kama zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hili nalo nilikuwa naomba liwe katika sheria hii ijioneshe kwamba fedha hizi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, marekebisho ya kifungu cha 30 yanasema kwamba kifungu hiki cha sheria mama kinarekebishwa kwa kupanga tena kifungu cha 30 kuwa 30(1) kama ifuatavyo:

“Kwa kushauriana na Afisa wa Forodha mfanyakazi wa bandari aliyepewa mamlaka atakataa kumpa nahodha wa meli yoyote kile cheti cha kuondokea au kuingia bandarini mpaka akiwa (b) amepokea cheti kutoka kwa mfanyakazi mwenye mamlaka wa Mamlaka ya Bahari Zanzibar kinachoeleza kwamba meli imepakia idadi ya abiria inayotakiwa tu”.

Hii ‘tu’ Mhe. Spika, naona iondoke na halafu iwe akiwa amepokea cheti kutoka kwa mfanyakazi mwenye mamlaka ya Mamlaka ya Bahari Zanzibar kinachoeleza kwamba meli imepakia idadi ya abiria inayotakiwa, nafikiria hii ‘tu’ kwa sababu tunajua meli lazima iende na idadi ya watu kwa hivyo inatosha kusema kwamba inayotakiwa.

Nikiendelea kinasema kuwa Mabaharia baada ya hiyo, inatakiwa mabaharia imepakia vizuri na iko katika hali nzuri kwa safari za baharini. Kwa kweli huku mbele kidogo Mhe. Spika, inanichanganya, basi ilikuwa iwe, “idadi ya abiria inayotakiwa na mabaharia“. Nafikiri inatosha haya maneno ya mbele yote kwa uoni wangu nahisi haina haja ya kusema hali nzuri na nini au kwa sababu ya baharini kwa sababu tunajua kwamba meli safari zake si nchi isipokuwa zinakuweko baharini.

Mhe. Spika, nikiendelea katika sehemu hiyo hiyo ya pili marekebisho ya kifungu cha 50, atakaeonekana katika jengo au sehemu yoyote ya shirika bila ya kuwa na kitambulisho halafu kuna koma, ruhusa kutoka kwa mfanyakazi aliyeidhinishwa atakaeonekana katika jengo au sehemu yoyote ya shirika bila ya kuwa na kitambulisho hapa ingeandikwa au ruhusa kutoka kwa mfanyakazi aliyeidhinishwa na huku mbele au bila ya kuwa na kati ya ruhusa na vyenginevyo. Nafikiri Mhe. Spika, hapa tungeiondoa.

Mimi vile vile nishukuru Mhe. Spika, baada ya hayo niseme kwamba vile vile serikali iyasaidie haya mashirika. Kwa sababu hivi karibuni tulikwenda Shirika la Bima na wakatoa matatizo yao kwamba mali za shirika mara nyingi na hasa majengo yanakuwa yanachukuliwa chukuliwa na tunajua kwamba mashirika haya ni lazima yawe na mtaji na mtaji ni zile mali zake. Kwa hivyo, pia niombe serikali kwamba isaidie haya mashirika kwa kuwathibitishia zile mali zao na isiwe kila mara zinachukuliwa na kukabidhiwa kwa taasisi nyengine. Kwa hivyo, kila mmoja huenda kwa mtaji wake.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani ahsante sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa ndani ya hali ya uzima na afya njema kwa kuendeleza majukumu yetu ya kisheria yanayotukabili.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea marekebisho yake ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri aliotuletea katika marekebisho haya jinsi ya vile vifungu ambavyo vimerekebishwa na *paper* yake aliyotuletea, kifungu cha sheria kabla ya marekebisho na

marekebisho yake na baada ya marekebisho pia akatueleza na sababu za marekebisho haya. Hii imetufanya wengi kujua madhumuni na sababu zilizomfanya Mhe. Waziri kutuletea marekebisho haya. Kwa hivyo, nashukuru na nampongeza sana kwa sababu mimi binafsi nimefahamu vya kutosha.

Mhe. Spika, vifungu tumevielewa vinavyofanyiwa marekebisho na ni kiasi cha kufanyiwa marekebisho kwa vile vilivyokuwa mwanzo na hivi sasa. Mhe. Spika, katika kifungu cha 30(1) kwa kushirikiana na Afisa wa Forodha mfanyakazi wa bandari aliyepewa mamlaka atakataa kumpa nahodha wa meli yoyote ile cheti cha kuondokea na kuendelea mbele.

Mhe. Spika, kifungu hiki ni kuwa mwanzo kilikuwa ni afisa wa bandari yoyote ile anaweza kukataa lakini hapa haya mashirikiano ni jambo zuri ambalo mtu yeyote unapompa madaraka peke yake la kushirikiana na mwenzake basi kutakuwa na tofauti kubwa na wanaweza kupata masuala mazuri ya mafanikio ya shughuli yao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naunga mkono vifungu hivi vinavyorekebishwa.

Lakini jengine kifungu kile cha 3(b) ikiwa amepokea cheti kutoka kwa mfanyakazi wa bandari Zanzibar kinachoaeleza kwamba, meli imepakia idadi ya abiria na mabaharia wanaotakiwa tu na imepakia vizuri na katika hali nzuri kwa safari za baharini.

Mhe. Spika, mimi hili hapa ningeomba kuwa sio kupokea kile cheti tu lakini pia na ukaguzi ndani ya chombo kile basi uwepo, kwani kupokea cheti tu peke yake haujatosha bila ya kuwa na ukaguzi maalum ambao unakaguliwa.

Jengine kifungu cha 50 atakayeonekana katika jengo au sehemu yoyote ya shirika bila ya kuwa na kitambulisho ruhusa kutoka kwa mfanyakazi anaidhinishwa au bila ya kuwa na hati ya ruhusa au vyenginevyo. Hili pia ni suala zuri Mhe. Spika, juu ya jitihada zao watu wa bandari wanazofanya lakini bado kuna uingiaji wa watu kiholela ndani ya meli hasa wale wanaopokea mizigo kwa wasafiri hasa katika Bandari yetu ya Mkoani. Kwa hivyo, mimi ningemuomba Mhe. Waziri hawa wahusika waliopo pale bandarini aidha wale wachukuaji wa mizigo au wengineo basi tuwatambue vizuri. Kwa sababu meli haijafunga gati vizuri basi watu wamesharukia kwenye meli zile na kufanya tafrani ndani ya chombo kile. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba hawa watu wawe na nembo maalum amabzo zitawaruhusu kufanya shughuli zao katika bandari zetu mbali mbali.
Mhe. Spika, katika kifungu cha 67 kwa kuzingatia vifungu vyengine vya sheria yoyote vinavyohusiana na fedha, waziri anaweza kutunga kanuni za fedha kwa ajili ya matumizi ya shirika. Kwa nini Mhe. Spika, hapa isiwe waziri atatunga kanuni na badala yake kusema waziri anaweza kutunga kanuni za fedha kwa ajili ya matumizi ya shirika. Mimi nigemuomba Mhe. Waziri hapa hiki kifungu kiandikwe kwamba, waziri atatunga kanuni za fedha kwa ajili ya matumizi ya shirika sio anaweza.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, mimi naunga mkono marekebisho haya kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu kidogo tu, kwa sababu mswada huu nadhani wenzangu wote wameshauchangia na kila mmoja anayesimama hapa anausifu mswada huu. Kwa hiyo, Mhe. Spika na mimi niseme kwamba hakuna kitu kizuri kama kusema na mwenzako akakusikia, vile vile hakuna kitu kibaya kama kusema na mwenzako akakupuuza.

Kwa hivvyo, Mhe. Spika nimpongeze Mhe. Waziri kwa marekebisho yake haya, ili kuweza kufanikisha matakwa ya Wazanzibari wote. Pia Mhe. Spika, niseme kwamba tunatunga sheria kufuatwa yale ambayo yanatakiwa. Kwa maana hiyo, nimuombe Mhe. Waziri sheria hii itekeleze ipasavyo na hivi sasa inatungwa sheria kwamba hatimaye inaachwa njiani na kufuatwa mengine ambayo hayakutekelezwa ipasavyo.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 6(a) kinachosema kwamba, “Kwa kushirikiana na Afisa wa Forodha mfanyakazi wa bandari aliyepewa mamlaka atakaa kumpa nahodha ile cheti cha kuondokea au kuingia bandarini mpaka...” hapa Mhe. Spika, niseme kwamba meli yoyote kile cheti, ningeomba itafsirike kwamba nahodha wa meli yoyote, itafsiriwe kwamba kwa kushauriana na Afisa wa Forodha mfanyakazi wa bandari aliyepewa mamlaka atakataa kumpa nahodha wa meli yoyote cheti cha kuondokea au kuingia bandarini. Hii kidogo Mhe. Spika, inanipa utatanishi.

Lakini pia Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 10 kinachosema kwamba, “Bodi itakuwa na wajibu wa kuteuwa Katibu wa Bodi miongoni mwa wafanyakazi wa shirika mwenye sifa ya kuwa na angalau na digrii ya kwanza ya

sheria pamoja na uzoefu wa kazi angalau miaka mitatu". Hii niseme nimpongeze Mhe. Waziri kwa bodi hiyo itakayokuwa hivyo, kwa sababu kuteuwa mtu mwenye digrii ya sheria itakuwa ni moja wapo katika huu mswada ni sheria. Nimpongeze Mhe. Waziri.

Lakini Mhe. Spika, niseme kwamba kwa kuwa mswada huu wengi wetu wameshauchangia na wameona ni mswada ni makini, na mimi nasema nampongeza Mhe. Waziri tena kwa mswada ambao ni mzuri na ambao utatufikisha pale ambapo tunapohitaji.
Lakini la mwisho niseme kwamba namuomba Mhe. Waziri yale ambayo yamerekebishwa katika mswada huu ikiwa atatokea mtu kuvunja sheria hii achukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba nikae kitako.

Mhe. Spika: Enaelekea tumefikia pazuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi sina budi kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu katika marekebisho ya sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Bandari, Sheria Na. 1 ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, kabla ya yote naomba nichukue nafasi kwa kusema kwamba naunga mkono marekebisho haya na mswada huu kwa asilimia mia moja kwa mia moja, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka.

Mhe. Spika, katika mswada huu kama ilivyoelezwa katika madhumuni na maudhui ya kuleta marekebisho haya, yameelezewa mambo matatu ambayo ni ya msingi katika kuona kwamba tunajenga taasisi yetu kwa malengo ya kuleta ufanisi, umakini na yale malengo ya upatikanaji wa tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nianze kwa kusema kwamba taasisi yetu hii ya Shirika la Bandari ni taasisi ambayo imekamata mlango mkuu wa kuhimili uchumi, ushindani na huduma kwa wananchi wa nchi ya Zanzibar. Malengo hayo na madhumuni hayo, sisi tukiwa kama sehemu ya serikali tunayatambua na tutahakikisha kwamba tunayatekeleza kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotujaalia kutupa nguvu.

Mhe. Spika, kwa kuanza kabisa naomba nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye amepongeza sana jitihada za serikali katika kufungua milango kwa kuona kwamba tunaweza kushirikiana na wawekezaji binafsi na wadau wa ushirika wa maendeleo katika kuimarisha huduma ya bandari kwenye bandari yetu ya Malindi.

Mhe. Spika, pamoja na Mhe. Hamza Hassan Juma na yeye ametaka kujua namna ya mwenendo, hatua na kama kuna mikataba yoyote iliopo kati ya serikali na mwekezaji ambaye anaendelea kuekeza katika eneo la *passengers terminal* kwenye bandari yetu ya Malindi.

Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba mwekezaji yule ni mzalendo, amekuja amezungumza na serikali kwa lengo moja tu la kutaka kuimarisha huduma kama alivyofanya upande wa pili wa Jamhuri katika bandari ya Dar es Salaam, ni kwamba tumekaa naye, tumezungumza naye na tumekubaliana.

Wajibu wetu sisi kama serikali ni kuona kwamba ile *master plan* ya bandari iliopo ndio inayosimamiwa kwa kushirikiana na taasisi nyengine kama Manispaa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kwa kuona kwamba ujenzi ule unaenda sambamba na mamlaka husika, lakini yanayofanyika pale yote yanapata baraka ya taasisi hizo tulizozitaja kwa malengo ya kuona kwamba hakuna kinachokiukwa. Hivyo nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba tunao mkataba na tunakwenda vizuri na tunashauriana kwa kila hatua ya ujenzi unaoendelea.

Mhe. Spika, suala la pili naomba nipokee pongezi za kutambua na kuimarisha huduma zetu kama Shirika la Bandari, kumekuwa na mkanganyiko hasa namna ya kupata hati ya mwisho inayoamuru chombo kuweza kuondoka katika bandari, na haya kweli yamethibitika kutokana na ajali ambazo zimetokezea pamoja na tume ambazo zimeundwa, ikaonekana jambo hili nalo pia linaleta mkanganyiko.

Lakini matarajio yetu kwamba baada ya kufanya marekebisho haya tutakuwa hivi sasa tumetanua wigo, uhusiano na ufanyakazi wa karibu zaidi kati ya taasisi mbili hizi, kwa maana ya ZMA na Shirika la Bandari, kwani hivi sasa

afisa wetu wa bandari atakuwa na mamlaka hivi sasa ya *concern* yake katika kuruhusu chombo kuondoka baada ya kukabidhiwa hati ile ambayo wamepewa lakini pia. Naomba nikubaliane aliyetoa Mhe. Mwakilishi baada ya kuona ipo haja ya yeye mwenyewe kuja kujiridhisha kabla ya kukubaliana na hati hiyo ambayo atakuwa amepewa.

Mhe. Spika, pia limeelezwa suala jengine katika *concern* ya Waheshimiwa Wajumbe suala la kifungu cha 30 ambacho kimerekebishwa kuhusiana na masuala ya forodha, lakini pia kifungu kinachoelezea namna ya mabadiliko ya kanuni ya fedha kuondoa mkanganyiko ambao uliokuwepo kati ya Mhe. Waziri pamoja na Bodi. Tumeona ni busara na ni vyema kwamba mamlaka haya yakapita kwenye bodi na mamlaka ya waziri yakabakia kwenye kanuni ambazo amezitunga.

Malengo ya kufanya hivyo ni kutambua kwamba Mhe. Waziri kila bajeti ya bodi inapokaa yeye ndiye mtu wa mwisho anayeidhinisha. Kwa hivyo hakutokuwa na usumbufu wala mkanganyiko wowote baada ya kwisha kuipitisha bajeti ile ya bodi tukaona kwamba hakuna haja ya mara ya pili Mhe. Waziri kuja kuingilia tena katika namna ya usimamizi na uendelezaji wa matumizi ya fedha katika shirika hili.

Mhe. Spika, imeelezewa pia suala la kuimarisha chelezo ambacho amezungumza Mhe. Hamza. Hili tumelipokea na kama jana tulivyojibu swali kwamba malengo ya kuimarisha chelezo kipo, chelezo chenyewe, vifaa lakini pia mafundi na wafanyakazii wa idara ile nao pia tuna malengo ya kuwaimarisha.

Tulichotukwaza hivi sasa kama tulivyoeleza kipa umbele chetu ni kutoa huduma zilizo bora zaidi kwa upande wa maeneo ya ushushaji, uwekaji wa maeneo ya kontena. Kwa hivyo malengo yetu ni kwamba tutakapomaliza *phase* ya kwanza kuimarisha sekta hizo, eneo la pili tutakuja katika kuimarisha chelezo chelezo chetu.

Mhe. Spika, pia limezungumzwa suala la uimarishaji katika eneo hilo la uwekaji wa makontena. Napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba malengo yetu ni kuona kwamba eneo hilo linaimarika, tunatambua changamoto ziliopo, kwani ni pamoja na upungufu wa fedha, upungufu wa vifaa lakini matarajio yetu ni kwamba tayari kwamba mwaka huu tuna vifaa ambavyo tutavipata na mwakani tutaendelea tena na bajeti kutafuta vifaa hivyo kadri ya hali inavyokwenda ndivyo hatua ya maendeleo itakapokuwa inaongezeka.

Mhe. Spika, limezungumziwa suala la watu ambao wana udhibiti wa watu wanaoingia katika kwenye eneo la bandari la mchana, nalo hili pia tumeliingiza katika mabadiliko haya kwa kutambua kwamba tumekuwa na matatizo, sheria yetu ilikuwa ikitambua wale watu wanaoingia katika bandari wasio na kazi maalum wala vibali na tulipokuwa tunapowakamata inakuwa usumbufu sana wenzetu wa Jeshi la Polisi, kwani sheria inawatambua wale tu watu wanaokamatwa nyakati za usiku na wakati wa mchana ilipelekea kwa watu wa Polisi kushindwa kuwashtaki kwa sababu sheria haikuwa wazi.

Kwa hivyo matarajio yetu baada ya kuona mabadiliko haya ambayo tumeingia hivi sasa itakuwa hata wale ambao wamekamatwa nyakati za mchana ambao hawana vibali wala ruhusa maalum nao sasa watakuwa wametenda kosa kwa mujibu wa sheria na hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao. Mhe. Spika, tunasisitiza kwamba suala la kuingia la vitambulisho na kufuata taratibu hili litaleta faida na manufaa kwetu sote.
Pia limezungumziwa suala la uuzaji wa tiketi kiholela Mhe. Spika, tunaomba kutoa wito kwa kuzitaka taasisi zinazotoa huduma lakini na wananchi wenzetu watambue malengo ya serikali ya kuona kwamba tunaheshimu taratibu zilizopangwa. Haitokuwa jambo la busara kuona kwamba serikali tunaendelea kupanga mikakati mizuri, wananchi wanaturejesha nyuma kwamba wao ni sehemu ya uvunjaji wa kanuni, sheria na taratibu ambazo zimepangwa.

Mhe. Spika, katika jambo la kushangaza mwananchi huyo huyo ambaye kwa hayo tunayoyalalamikia hapa, yeye mwenyewe binafsi haheshimu taratibu. Tumeelekeza mara nyingi tu kumtaka mtu kwamba aende na kitambulisho, usikubali kununua tiketi iliyokuwa ipo mikononi lakini wananchi hao wamekuwa ndio washirika wakubwa ya watu wanaofanya biashara ya magendo katika wale wanaouza tiketi hizi mikononi.

Nnachoweza kulihakikishia Baraza lako tukufu Mhe. Spika, tumelipokea *concern* hii tutaendelea kulifanyia kazi na tutaziomba vikosi na taasisi zetu husika nazo pia zitusaidie, kama vile Manispaa, watu wa ZRB, jeshi la Polisi na kadhalika.

Mhe. Spika, pia nimeona *concern* ya Mhe. Abdalla Juma Abdalla ya kurekebisha lugha. Nadhani nalo hilo sio jambo baya, pengine Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ataeleza kwa kina kuhusiana na jambo hilo.
Mhe. Spika, nakubaliana na *concern* ya Mhe. Hija Hassan Hija ya namna ya kuweza kudhibiti na kutumia mamlaka haya ambayo inapewa bodi kwa tahadhari kubwa kwa kutambua malengo ya serikali, kudhibiti na kuhudumia wananchi na sio ubadhirifu na matumizi yasiyokuwa halali kwa fedha za umma. Matarajio yangu kwamba bodi na mkurugenzi mkuu watakuwa wamelisikia na watalifanyia kazi kadri hali itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, jengine limezungumziwa suala la kifungu cha 50 kuhusu suala la watu wanaoingia kwenye maeneo wakati wa mchana, tayari nimeshaelezea lakini pia kuna *concern* ya Mhe. Bikame ambaye angependa suala la utungaji wa kanuni lisiwe kwamba ata, haya naamini Mhe. Waziri atakuja kuyatolea ufafanuzi wa kutosha.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Spika, niombe tu kwa Waheshimiwa Wajumbe wakubaliane na rai ya serikali na maoni ya serikali ya kuja kufanya mabadiliko haya ya sheria ili kuweza kupata sheria yetu hii iweze kuwa na nguvu zaidi za kusimamia kwa malengo ya kuleta ufanisi na tija kwa wananchi tunaowaongoza.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, naomba nirejee tena kwamba mimi mwenyewe binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka tunaunga mkono sheria hii asilimia kwa mia.

Mhe. Spika, nakushukuru.
Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mswada huu sio mkubwa ni mfupi na sina hakika kama waziri anaweza kuwa tayari hivi sasa kutoa majumuisho, pengine tukaongeza muda kidogo jioni tukapumzika. Nna wasi wasi tukiakhirisha hatutoweza kufika mapema kuipata *quorum* iliopo hivi sasa kupitisha huu mswada.

Kwa hivyo kama Mhe. Waziri ataniambia yupo tayari, mimi nitaomba sana tutapofika pahala kama muda umepungua kidogo tuzidishe lakini tumalize hii kazi, jioni tumpumzike.

Mhe. Waziri hebu twambie, upo tayari kufanya majumuisho au tuje jioni.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tufanye jioni.

(Saa 6.35 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11. 00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikaingia ndani ya wakati. Pili nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa majumuisho kwa mswada wetu huu wa Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari, Sheria nambari Moja ya mwaka 1997.

Kwanza napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote kwa utulivu uliopatikana katika mswada wetu, tokea mwanzo ulivyoanza kuchangiwa mpaka mwisho. Pili napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliochangia kama ifuatavyo;

1. Mhe. Salma Mussa Bilali amechangia kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, namshukuru sana. Pia nashukuru mchango wa Kamati kwa kutuunga mkono katika mswada wetu huu wa marekebisho ya sheria.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye yeye ni Mwenyekiti wa hii Kamati, lakini amechangia binafsi.
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Hamza Hassan Juma
5. Mhe. Ali Salum Haji
6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Bikame Yussuf Hamad

Hawa ndio ambao wamechangia leo. Napenda nimshukuru sana Naibu Waziri Mhe. Issa Haji Ussi Gavu kwa mchango wake aliotoa wa kufunga dimba lile la uchangiaji wa mswada. Ila napenda niombe radhi sana, lakini nimtaje Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi ambaye alichangia mwisho kabisa kabla ya kumpa nafasi Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, kabla sijaenda kwenye michango ya Mjumbe mmoja mmoja, ambayo kama ni mitano inataka ufafanuzi. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote waliozungumza kwa kuunga mkono hoja zetu, kwamba zina uzito na ni hoja ambazo ni kweli zinahitajika kufanya marekebisho katika uendeshaji mzima wa Shirika la Bandari.

Pili, nilipongezwa kuhusiana na *document* ambayo tuliisambaza iliyoainisha kwa njia ya bango kitita au *matrix* ile sheria kongwe iliyokuweko, marekebisho yaliyotolewa na sheria mpya inavyosema na sababu ya kurekebishwa. Napenda kupokea pongezi hizi, lakini na mimi kwa upande wangu, napenda niwashukuru sana na niwapongeze wanasheria wa Shirika la Bandari, pamoja na mwanasheria wetu wa wizara kwa kusikiliza maelekezo yaliyotolewa na Wajumbe hapa na wakaweza kufuata na kutoa muongozo ule ambao umewasaidia sana Wajumbe.

Mhe. Spika, kwa sababu hawa wanasheria wanalelewa, napenda nimpongeze sana Mkurugenzi wa Shirika la Bandari na Katibu Mkuu kwa kuweza kuwalea wanasheria wetu ili waweze kufuata ile miongozo. Baada ya hayo Mhe. Spika, napenda nitoe ufafanuzi kidogo kuhusiana na baadhi ya masuala ambayo yametolewa.

Mhe. Spika, tunakubaliana na wale Wajumbe waliosema kwamba pale panapotokea mgongano baina ya ile sheria iliyoandikwa kwa Kiingereza na ile iliyoandikwa kwa Kiswahili basi masahihisho yafanyike ili ile mantiki iweze kupatikana kama ambavyo ilitarajiwa katika sheria iliyoandikwa kwa Kiingereza. Kwa hivyo, tunaomba hapa tukubali kwamba pale ambapo lilitokezea tatizo hilo tunakubali kuwa patiwe masahihisho.

Kwa mfano, kuna kifungu kimeandikwa ‘Mamlaka ya Baharini’ ni ‘Mamlaka ya Usafiri Baharini’. Kwa sababu mamlaka ya bahari ni kubwa, inaweza kuwa na kila kitu, hata uvuvi ni mamlaka ya bahari. Hapa sisi tunazungumza mamlaka ya usafiri baharini.

Mhe. Spika, jengine nakubaliana na wazo la Mhe. Bikame Yussuf Hamad, kwa suala la kutunga kanuni zinazohusiana na fedha, Waziri sio anaweza kutunga. Isomeke atatunga kanuni, kwa sababu ni wajibu kutunga kanuni kwa mujibu wa taratibu za kifedha.

Mhe. Spika, masuala mengine ambayo yamejitokeza, la kwanza ni pongezi zilizotolewa kuhusiana na kifungu cha usalama na udhibiti wa bandari. Tunazipokea pongezi hizi na tunawahakikishia kwamba muhali kama ulivyotajwa na baadhi ya wajumbe utaondolewa, ili bandari yetu iwe salama na inayoweza kudhibitiwa kwa sababu kuna maisha ya watu, kuna mali za watu na kuna kila kitu ambacho kinatakikana pale.

Mhe. Spika, tukizungumza bandari, tukizungumza uwanja wa ndege tayari tunaingia katika suala la kimataifa sio tena suala la ndani tu. Kwa hivyo, tunaomba vile vile Wajumbe watuunge mkono katika suala hili ili wananchi wetu waweze kupata taaluma kikamilifu kuhusiana na usalama na udhibiti wa bandari.

Mhe. Spika, tuliulizwa swali hapa kuhusiana na ujenzi wa *terminal* ya abiria inayojengwa sasa hivi. Mhe. Spika, napenda nitoe ufafanuzi kwamba pale pana miradi miwili. Mradi mmoja ulikuwa ni mkubwa wa kuitengeneza ile bandari yote ili baada ya kupata Bandari ya Mpigaduri, basi bandari ile iachiwe iwe zaidi inafanya kazi za kushusha abiria na mizigo ya ndani. Bandari ya Mpigaduri iweze kufanya shughuli za kushusha mizigo na kupakia mizigo ya nje. Hii bado haijatekelezwa, bado mkataba uko katika meza na unajadiliwa. Kinachofanyika pale ni ufadhili uliotolewa na mfanyabiashara maarufu bwana Bakhressa wa kuweza kuweka nafasi ya abiria wetu kuweza kushuka kwa usalama, kuweza kupata pahali wakakaa kwa utulivu na kwa mpango. Haya ni makubaliano baina ya Shirika la Bandari na mfanyabiashara huyu.

Lakini pia napenda kusisitiza kwamba bado ujenzi ule unaoendelea na Shirika la Bandari bado halijakabidhiwa nafasi ile, mara tu baada ya ujenzi kukamilika utakaochukua vile vile nafasi ya kukaa VIP basi utakabidhiwa kwa shirika na uendeshaji wote utakuwa chini ya Shirika la Bandari. Gharama ya mradi ule unakisiwa kuwa shilingi milioni 800 ukikamilika. Lakini hata hivyo vyombo vyote ambavyo vinatumia bandari bado vinalipa kama kawaida inayotakiwa.

Mhe. Spika, kuhusu uteremshaji wa mizigo katika *terminal* hii ya abiria. Boti zetu zinazotoka Pemba au Dar es Salaam, zinabeba abiria na mizigo ya abiria, ile yote inateremshwa na kuna vitoroli maalum vilivyowekwa sasa hivi kwa ajili ya kuteremsha mizigo, ambapo vitoroli vile vina uwezo wa kupita kwenye *tiles* bila ya kuleta taathira.

Hii boti ya *Flying Horse* Mhe. Spika, inachukua mizigo ya aina mbili. Inabeba mizigo ya abiria ambayo wanaruhusiwa kushusha pale na vile vile inabeba mizigo ya kibiashara. Sasa mizigo ile ya kibiashara hata ile *terminal* yenyewe hai-*support*, achilia mbali ya *tiles*, hata ile *gate* yenyewe hai-*support* kushusha pale. Kwa hivyo, ndio mizigo ile mizito ya kibiashara inaambiwa boti ikashushe katika *gate* kubwa, kwa manufaa ya ile *gate* yenyewe na kwa maslahi ya wananchi wote kwa jumla. Kwa hivyo, ni ile mizigo mizito ya kibiashara ndio ambayo boti ile inachukua ya *Flying Horse* inayoelekezwa kushusha katika bandari kubwa na sio kushusha katika bandari ndogo ya abiria.

Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Mjumbe wa kuona kwamba baada ya kukamilika kunawekwa *carpet* au zulia ambalo litarahisisha kupita vile vitoroli, limechukuliwa na Shirika la Bandari na linafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba bandari yetu imeanza kupata mizigo mingi zaidi kuliko ambavyo ingetarajiwa. Meli kubwa zinakuja sasa hivi zenye kontena kuanzia 300 mpaka 400 kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, ni kweli kwamba uwezo wa kushusha ulikuwa ni mdogo. Lakini nalihakikishia Baraza hili, kwamba ndani ya mwisho wa mwezi wa Machi tuliweza kupata, baada ya kuiagizia *reach staker* nyengine mpya, ambayo sasa imemaliza lile tatizo la meli kubaki muda mrefu katika *gate* yetu. Hata hivyo, kuna matatizo mengine ambayo yanajitokeza kwamba kontena hizi, inabidi kutokana na nafasi iliopo zipangwe nne kwa pamoja.

Kwa hivyo, bado baadhi ya wafanyabiashara wanapata usumbufu wa kupata kontena zao kwa muda mfupi, kutokana na kwamba zile kontena zinakaliana na ile ya chini ambayo inahitajika sio rahisi kuipata kwa muda huo. Kwa hivyo, tunawaomba wafanyabiashara na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawe wavumilivu, sasa hivi kazi zinazoendelea ni kuongeza sakafu ya eneo la kuweka kontena, ili ziweze kusambazwa kwa vizuri zaidi. Hivi karibuni tutaanza mradi wa ujenzi wa ofisi ya Shirika la Bandari ambayo itajengwa katika lile jengo lililokuwa la vioo, lile lililokuwa la Wairaq. Ikipatikana nafasi ile, nafasi iliyokuwa ofisi mabanda yote yanaweza kuwa ni sehemu ya kuwekea kontena vile vile. Kwa hivyo hali hii tunakwenda hatua kwa hatua na nina amini kwamba tutafikia wakati kuwa pamoja na udogo wa bandari yetu, lakini tunaweza kuwa na nafasi nzuri za kuweza kuweka kontena na zikakaa kwa mujibu wa mpango.

Mhe. Spika, tunajua kwamba suala la kudumu ni la kupata bandari kubwa zaidi ilioko Mpigaduri. Serikali inafanya jitihada zote katika kuona kwamba tunapata wafadhili au wawekezaji katika kujenga bandari hiyo. Imetamka wazi serikali kwamba iko tayari kufanya (BOT) yaani *Build Operate and Transfer*, lakini wawekezaji wana masharti yao na serikali ina masharti yake. Kwa hivyo, hapo itakapofikia wakati tukalingana masharti ya mwekezaji baada ya mazungumzo na masharti ya serikali, basi serikali itatoa nafasi ile ya kujenga.

Mhe. Spika, wengi wameshajitokeza sasa hivi, lakini hapo itakapofika wakati wa kuona kwamba makubaliano yamefikiwa, basi tutazungumza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kuhusu eneo la Saateni Shirika la Bandari halikupewa tu lile eneo limekodishwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma atustahamilie sana, atuvumilie kwa hapo, kwa sababu sisi tumelikodi, kwa hivyo ziko kazi zinapangwa kwa ajili ya eneo hilo na labda aende kwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili kupata eneo jengine kwa ajili ya Jimbo lake la Kwamtipura.

Mhe. Spika, kuhusu bidhaa mbovu zinazoingia bandarini, Mhe. Spika, bidhaa mbovu hasa za vyakula na vipodozi zinapoingia bandarini utaratibu wake ni kwamba bodi ya chakula na vipodozi iliopo chini ya Wizara ya Afya, ndio dhamana ya kuishughulikia bidhaa ile na mwenye mali yule ikishakaguliwa bidhaa ikaonekana kwamba hii haifai kwa binadamu anapewa taarifa akaiangamize ile bidhaa. Akishindwa katika kipindi maalum, basi bodi ile ina dhamana ya kuichukua bidhaa ile na kuiangamiza na gharama ya kuangamiza bidhaa ile atalipa yule ambaye ameleta bidhaa ile.

Kwa hivyo, taratibu ziko sasa katika mchakato mkubwa, wale ambao waliuliza kwa unga ule mbovu uliopo. Utaratibu katika hali ya juu kabisa ya kushughulikiwa ili bidhaa ile iondoke pale na kuangamizwa, ambapo

ikikamilika bidhaa ile haiwezi kukaa, kwa sababu bandari inakula hasara sana ikiwa kutawekwa bidhaa ambayo haifai katika bandari ile. Kwa sababu kila siku inapokaa bidhaa ile inaitia hasara Shirika la Bandari na malipo yale inabidi yamrudie yule ambaye ameiweka ile bidhaa. Sasa utaratibu huu utafuatwa Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba bidhaa zinazoingia na ambazo hazifai kwa binadamu kwa mujibu wa bodi ya chakula na vipodozi ichukue muda mfupi iwezekanavyo kuondoka bandarini.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba sasa nichukue fursa hii kuwashukuru tena Wajumbe wote na kuwaomba kwamba kwa sababu wamekiri wenyewe kwamba mswada wa marekebisho ni mdogo, umekuja kwa wakati na umelingana na hali ilivyo. Kwa heshima na taadhima naomba Wajumbe waupitishe na Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya kutunga sheria, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar ya Mwaka 2013

Sehemu ya Kwanza
Masharti ya Awali

Kifungu 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika.

Kifungu 2 Kusomwa.

Sehemu ya Pili
Marekebisho

Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha 11

Kifungu 4 Marekebisho ya Kifungu cha 13

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kupata ufafanuzi wa ziada. Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa jawabu nzuri ambayo amenijibu, nategemea wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura ambao karibu asilimia 35 ya wakaazi wangu ni wachukuzi. Kwa hivyo, kile kilio chao cha kuwekewa lile *carpet* au zulia, kwa kuwa Mhe. Waziri amekitolea kauli na kwa kuwa amesema kwamba uongozi wa Shirika la Bandari utaweza kulishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa *veteran*, yaani nilikuwa ni mjumbe wa bodi naamini hawatoweza kuniamini, ili wananchi wangu waendelee kuniamini kwamba ninawatetea. Isipokuwa tu kidogo nilikuwa nahitaji maelezo kwa faida yetu sote, kwamba sijui kama sikusikia vizuri au vipi, angenisaidia kwamba ule uwekezaji yaani zile gharama hasa za ule ujenzi anashughulikia nani. Kama yule mjenzi mzalendo ambaye tumekubaliana kwamba utaratibu wa BOT kuwa je, zile gharama atakuja kulipwa au amejenga kwa uzalendo au gharama zile ni za Shirika la Bandari, yeye anakuwa ni mjenzi tu. Kwa hivyo, kidogo nilikuwa nataka nipate ufafanuzi katika eneo hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu katika jibu mama kwamba huyu ni mfadhili wa ndani, na ni kwa uhisani anatujengea. Sisi tumeshuhudia kwamba pale Dar es Salaam

iko *terminal* ile na abiria wanapumzika na hapa lengo lake ni kwamba itakuwa chini ya Shirika la Bandari. Kwa hivyo, haitokuwa katika dhamana yake, akimaliza kujenga fursa yote ile anaikabidhi Shirika la Bandari ndio watakaoweza kuishughulikia. Kwa hivyo, ule ni ufadhili tu ambao ametoa na baadae kuwapa Shirika la Bandari. Kwa sababu huko nyuma kulikuwa na dhana kwamba yeye ndiye atakayekuwa *controller* wa kila kitu, lakini hiyo imewezekana kwamba Shirika la Bandari ndio litakaloshughulikia maeneo yale. Ndio maana ikawepo hiyo sehemu ya VIP kwa wale abiria ambao wanasafiri kwa njia ya boti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli hiyo ya Mhe. Waziri, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana mfadhili huyo wa ndani na tunamshukuru sana, awe na moyo wa kutusaidia wananchi, hasa baada ya kutuona kwa muda mrefu tunapata tabu tunaposafiri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa kupitia Baraza hili, naomba mpelekee salamu zetu za dhati kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao sote hapa naamini tutaweza kutumia eneo lile. Sio yeye tu, na wengine kama wapo vile vile watakuwa na moyo wa kizalendo kama huu, basi pia tunamuomba Mhe. Waziri awakaribishe ili nchi yetu iweze kupiga hatua za maendeleo. Ahsante sana.

Kifungu 4	Marekebisho ya Kifungu cha 13
Kifungu 5	Marekebisho ya Kifungu cha 23
Kifungu 6	Marekebisho ya Kifungu cha 30 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 7	Marekebisho ya Kifungu cha 50 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 8	Marekebisho ya Kifungu cha 60 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 9	Marekebisho ya Kifungu cha 67.
Kifungu 10	Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Niwahoji sasa Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar ya Mwaka 2013

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Shirika la Bandari la Zanzibar ya mwaka 2013 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada katika kuusoma mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, shughuli za leo mmezimaliza vizuri. Nichukue nafasi basi kuwashukuru kwa kazi hiyo nzuri mliyoifanya na kwa kuwa hakuna ziada yoyote, basi niakhirishe kikao hiki hadi kesho siku ya Ijumaa, tarehe 05/04/2013 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 11:30 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 05/04/2013 saa 3:00 za asubuhi)